


Jumatatu Oktoba 9, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581458
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



UMEME WA RATIBA

# Shubiri kwa maseremala

• **Kilio** chasikika hadi kwa mafundi cherehani, wachomelea vyuma... *Endelea ukurasa 5*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**TRA** yabaini stempu bandia, mmiliki kampuni mbaroni

UKURASA WA 7
**Biteko** azindua mpango wa kutangaza vivutio vya utalii



UKURASA WA 8
**CTI** yapata mbinu kuongeza masoko kimataifa bidhaa kutoka Tanzania

## Bei ya petroli, dizeli yazidi kupaa Zanzibar

UKURASA 17



Fundi cherehani Aisha wa Goba, Ubungo mkoani Dar es Salaam akiwa katika eneo lake la kazi jana, akidai kuchelewesha nguo za wateja kutokana na kutokuwa na uhakika wa nishati ya umeme. **PICHA: MIRAJI MSALA**



## Samia kutunukiwa shahada udaktari wa heshima India

UKURASA 2

**MICHEZO** GAMONDI AKATAA MECHI CAF, AITAKA AZAM UK.24 **KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA



Mbunge wa Muheza mkoani Tanga ambaye ni Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma, akizungumza na mmoja wa wazee baada ya kuhutubia mkutano wa hadhara jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Samia kutunukiwa shahada udaktari wa heshima India

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan kesho atatunukiwa Shahada ya Udaktari ya Heshima na Chuo Kikuu cha Wharlal Nehru cha India kutambua mchango wake wa kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia baina ya nchi hizo mbili.

Rais Samia jana alianza rasmi ziara ya kitaifa ya siku nne India kwa mwaliko wa Rais wa nchi hiyo, Droupadi Murmu, yenye lengo la kuendeleza kudumisha uhusiano uliopo kati ya nchi hizo.

Kiongozi huyo aliwasili nchini India jana alasiri kwa ajili ya ziara hiyo ya siku nne kuanzia jana hadi Oktoba 11 mwaka huu.

Ushirikiano kati ya nchi hizo umejikita katika sekta za kimkakati ikiwamo za afya, viwanda na biashara, ulinzi na usalama, elimu, teknolojia ya habari na mawasiliano, uchumi wa buluu, maji na kilimo.

Akizungumzia shahada hiyo jana, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, alisema hafla hiyo itafanyika kesho katika chuo hicho ikilenga pia kutambua mchango wa Rais Samia katika kusukuma maendeleo ya sekta zinazogusa jamii moja kwa moja ikiwamo uchumi. "Wanatambua mafanikio katika utangamano wa kikanda, kuimarisha uhusiano wa kitaifa kwa ujumla kwenye umoja wa taifa. Kwa hiyo, sisi tunashukuru kwamba Mheshimiwa Rais anatambuliwa na anaheshimika kwa kazi kubwa anayofanya na mchango mkubwa anaotoa," alisema January.

Hiyo ni shahada ya pili ya udaktari wa heshima kutolewa kwa Rais Samia tangu aingie madarakani Machi 19, 2021. Novemba 30 mwaka jana, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kilimtunuku Shahada ya Udaktari wa Falsafa ya Heshima kutokana na mageuzi ya kiuchumi na matumaini mapya kwa Watanzania kwa kuboresha elimu.

Katika ukurasa wake wa kijamii wa Instagram, Ikulu ya Tanzania ilieleza jana kuwa lengo lingine la ziara hiyo ni kutangaza fursa za biashara na uwekezaji za Tanzania, ili kuvutia uwekezaji na wafanyabiashara kutoka India.

Kwa mujibu wa Ikulu, ushirikiano wa miaka 62 wa nchi hizo unaendelea kuiletea nchi manufaa ikiwamo India kuwa mdau mkubwa wa maendeleo nchini, ikishika nafasi ya tano kwa uwekezaji.

Kwa mujibu wa Ikulu, hali hiyo imesababisha ongezeko la biashara kati ya nchi hizo kufikia Dola za Marekani bilioni 3.14 mwaka 2022 kulinganisha na Dola bilioni 2.14 mwaka 2017.

Ushirikiano wa kibiashara kati ya nchi hizo pia umechangia kuwapo ongezeko la mapato kutoka Dola bilioni 2.1 mwaka 2017 hadi kufikia Dola 3.1 mwaka 2021/22, huku miradi ya uwekezaji 630 yenye thamani ya Dola bilioni 3.74 ikisajiliwa nchini kati ya mwaka 2021 na 2022.

Kupitia ushirikiano huo, Tanzania imetekeleza miradi mikubwa ya maji kupitia ufadhili wa India, ikiwamo mradi wa maji wa Tabora -Ingunga-Nzega uliogharimu Sh. bilioni 617 ambao umekamilika na wa miji 28 wa Sh. trilioni 1.48 unaoendelea kutekelezwa.

Tanzania pia inanufaika na fursa za mafunzo ya muda mfupi na mrefu kupitia mradi wa teknolojia na uchumi pamoja na Baraza la Uhusiano na Utamaduni la India tangu mwaka 1972.

Vilevile, India inaanzisha kampasi yenye hadhi ya juu ya Chuo cha Teknolojia (IIT) Madras, Zanzibar, inayotarajiwa kuanza mwezi huu.

India pia imetoa mkopo nafuu wa Dola za Marekani milioni 500 kutoka Benki ya Exim unaotumika kuboresha huduma ya maji katika miji 24 nchini.

Ziara hiyo ni ya kwanza kwa kiongozi wa kitaifa kutoka Tanzania kutembelea India tangu mwaka 2015. Kwa upande wa India, mara ya mwisho kiongozi wake kuzuru nchini ilikuwa mwaka 2016.

Ikulu ilieleza kuwa uhusiano wa kidipolasia kati ya nchi hizo mbili ulianza mwaka 1961, India ilipofungua ubalozi wake nchini na Tanzania kufungua wake India mwaka uliofuata. Tangu kipindi hicho nchi hizo zimeendeleza urafiki na ushirikiano katika masuala mbalimbali.

Mwishoni mwa wiki, Waziri January, akizungumzia ziara hiyo, aliwaambia waandishi wa habari kuwa India inatarajiwa kuanzishwa taasisi ya upandikizaji figo nchini pamoja na kiwanda cha kutengeneza chanjo za binadamu na wanyama.

## Tanzania yaanza maandalizi ushiriki Mining Indaba 2024

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kupitia Wizara ya Madini kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Madini imeanza maandalizi ya kushiriki maonesho makubwa ya madini barani Afrika 'Mining Indaba'.

Taarifa iliyotolewa na Wizara ya Madini, imesema maonesho hayo yatakayofanyika mwezi Februari, mwakani katika Jiji la Cape Town, nchini Afrika Kusini yatashirikisha wafanyabiashara, watoa huduma, taasisi mbalimbali za kisekta pamoja na wakuu wa kampuni kubwa za uchimbaji madini duniani.

Akizungumza wakati akiwasilisha mpango wa ushiriki wa Tanzania katika maonesho hayo kwa Waziri wa Madini kwa niaba ya sekretarieti ya maandalizi, Mwenyekiti wa Chemba ya Migodi, Mhandisi Philbert Rweyemamu, alisema ni moja ya maonesho ambayo huwakutanisha wawekezaji wapatao 900, taasisi za sekta 40 na watendaji wa kampuni 1000.

Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, alisema ushiriki wa Watanzania katika maonesho hayo unatarajia kuiweka Tanzania kwenye ramani ya Afrika na dunia huku ukileta sauti moja kwa wadau kuielewa.

Katibu Mkuu Wizara ya Madini, Kheri Mahimbali, alisema dhamira ya wizara ni kuweka ushiriki wa pamoja katika banda moja la wizara, taasisi na wadau ili kufanya ushiriki wenye tija zaidi kwa Tanzania.

Tanzania inatarajia kutumia maonesho ya Mining Indaba kuvutia mitaji, uwekezaji, kujifunza, kuleta teknolojia bora za uchimbaji, kujenga mahusiano ya kibiashara, kuimarisha ushirikiano pamoja na mambo mengine.

Kampuni zinazotarajia kudhamini ushiriki wa Tanzania katika maonesho hayo ni pamoja na Anglo Gold Ashanti, Barrick Gold, Shanta Gold, Mantra Tanzania, Tembo Nickel, TRX Gold, Petra Diamond na City Engineering Ltd.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na. 70/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU ZUBEDA IDRISA MKONDO wa MPAMAA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA RAMADHANI SALUMU RAMADHANI**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 06 Mwezi 11 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 06 Mwezi 10 Mwaka 2023.

**KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA**



**GROLY DAVID MAKOYE** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba **TAE 077934** iliyotolewa makao makuu Dar es Salaam **PCO** mwaka **2018.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/DAILA/21757/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na. 69/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU ALLY SAIDI NDEE wa ....**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA HAMADI SAIDI NDEE**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 19 Mwezi 10 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 05 Mwezi 10 Mwaka 2023.

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTATION COUSE 112 OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE BLANDINA JUVENAL NAMWATTA**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR GTANT OF LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**JUVENAL MANYUNGA NAMWATTA .............PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN. 10 OF 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of the letters of administration is made to the above named petitioner
Objections to the grant should be filed on or before the 23rd day of October, 2023
Dated at Dodoma this 03rd day of October, 2023
Dated at Dodoma this 03rd day of October, 2023

**KUPOTEA KWA CHETI**



**DISMAS EMMANUEL MANYIKA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **Index No. S.1261/0060** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MERRIWA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016. Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya Polisi: **DOD/CHA/RB/133189/2023**

# Waziri ataka kasi upandaji miti

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Dunstan Kitandula, ametoa wito kwa Watanzania kuongeza kasi ya upandaji miti katika maeneo yao.

Alitoa rai hiyo juzi jijini Dar es Salaam alipofunga Kongamano la Tatu la Kimataifa la Viongozi Vijana na Mabadiliko ya Tabianchi lililokutanisha washiriki vijana kutoka nchi 24 duniani.

"Na pale tunapokata mti tuhakikishe tunapanda ili mwisho wa siku wote tuwe salama na mabadiliko ya tabianchi yanayoikumba dunia kwa sasa," alisema Kitandula.

Alisema kasi ya ukataji miti ni kubwa. Utafiti unaonesha asilimia 90 ya nishati inayotumika inatokana na miti hiyo.

"Kwahiyo, kama nchi tumeliona hilo na ndio maana Rais Samia Suluhu Hassan mwaka jana alizindua mkakati wa matumizi ya nishati safi na salama.

"Mkakati huu unaelekeza namna ya kutumia vyanzo vingine mbadala vya nishati safi na kuondokana na matumizi ya mkaa, tayari serikali imeelekeza kwamba katika eneo lolote lenye watu wasio chini ya 200 au 300 nishati inayotakiwa kutumika ni safi na salama.

"Na katika hili tunapongeza sana Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) kwa kazi kubwa wanayofanya kuhakikisha miti inapandwa na inatunzwa na katika kongamano hili wamewezesha vijana kupanda mikoko katika fukwe zetu. Mikoko inasifika sana katika kutunza hewa ukaa na kurejesha uoto wa asili ambao umetoweka," alisema.

Kamishna wa Uhifadhi wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo, alisema mbinu kubwa wanayoitumia katika kufanikisha na kufikia malengo waliyojiwekea katika kupanda miti na kupambana na uharibifu wa mazingira ni kuishirikisha jamii hususani vijana.

"Kwa maana hiyo tunawapatia ujuzi wa kutumia sekta hii ya misitu na uhifadhi wa mazingira kujipatia kipato na wakati huohuo wanakuwa wanahifadhi misitu.

"Kwa mfano, tunawapa vijana maeneo wanafuga nyuki na hata katika maeneo ambayo tunapanda miti hiyo nako tumekuwa tunawapa wafuge nyuki," alisema Prof. Silayo.

Shamim Nyanda, mwanaharakati wa mazingira, alisema kupitia kongamano hilo, vijana wamejengewa uwezo wa namna ya kuanzisha miradi ya utunzaji mazingira.

"Na tumejengewa uwezo kwamba tunapoanzisha miradi hiyo, tufahamu namna ya kuikuza na kuiendeleza na ilete matokeo chanya katika jamii au nchi zao," alisema Shamim.

# Serikali yatoa kibali wananchi kulipwa fidia ya mabilioni

**Na Mwandishi Wetu,** MASWA

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, amesema serikali imetoa kibali cha Sh. bilioni 16.2 kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha ujenzi wa miradi ya barabara kote nchini.

Bashungwa alibainisha hayo mkoani Simiyu baada ya kukagua mtandao wa barabara mkoani humo na kujionea utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya mchepuo (Maswa Bypass) yenye urefu wa kilometa 11.3 kwa kiwango cha lami ambao ujenzi umefikia asilimia 99.

"Mheshimiwa Rais ameshatoa zaidi ya Sh. bilioni 16 kwa ajili ya kulipa madeni ya fidia ya kuishia Juni 30, 2023. Dhamira ya dhati aliyonayo ni kuhakikisha mtandao wa barabara nchini unaimarishwa," alisema Bashungwa.

Waziri huyo alisema lengo la serikali kuijenga barabara ya mchepuo ya Maswa (Maswa Bypass) ni kupunguza msongamano wa magari yanayopita katikati ya Mji wa Maswa.

Alisema serikali tayari imetenga fedha kwa ajili ya kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Bariadi-Salama-Mhayo-Magu (Km 76), Bariadi-Itilima-Mwandoya-Moroco (Km 104), Nyashimo-Ngasamo-Ndutwa (Km 48) ili kupata gharama za ujenzi wake kwa kiwango cha lami.

Akitoa taarifa ya mradi, Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Simiyu, John Mkumbo, alieleza kuwa mkataba wa ujenzi wa barabara hiyo ulitiwa saini kati ya TANROADS na Mkandarasi - Kampuni ya CHICO Juni Mosi 2021 kwa gharam ya Sh. bilioni 13.4.

Aliongeza kuwa mkandarasi anaendelea kumalizia kazi ndogo za kuweka alama za barabarani, kuchora mistari ya usalama barabarani na kujenga miundombinu saidizi ya barabara.

# Azma kuzalisha tani 700,000 za korosho yaundiwa mkakati

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

SERIKALI imeweka lengo la kuwa na uzalishaji wa tani 700,000 za korosho kwa msimu kufikia mwaka 2025, ambao ni ukomo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Juni 1999-2025.

Kufanikisha azma hiyo ya serikali, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, amebainisha mikakati ya kuchochea kasi ya uzalishaji wa zao hilo kupitia huduma za kibenki mahususi zinazoendana na mahitaji ya wakulima.

Alibainisha mikakati hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa hafla ya uzinduzi wa kampeni maalum kwa wakulima wa korosho katika mikoa ya Mtwara na Lindi.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na wadau mbalimbali wa zao hilo wakiwamo viongozi wa kiserikali, viongozi vyama vya msingi (AMCOS), vyama vikuu vya ushirika, maofisa wa Benki ya NBC na wakulima wa zao hilo mkoani Mtwara.

Kanali Abbas alisema kampeni hiyo inayoitwa 'Wekeza NBC Shambani Ushinde', imekuwa na mchango mkubwa kwa wakulima kutokana uwekezaji mkubwa wa elimu ya fedha uliombatana na kampeni hiyo sambamba na aina ya zawadi zinazolenga kuchochea kasi ya uzalishaji wa zao hilo ikiwamo zawadi kubwa za matreka.

"Kampeni hii ikiwa kwenye msimu wake wa tatu, binafsi nimeona mabadiliko yenye tija miongoni mwa wakulima ambayo ninaamini kwa kiasi kikubwa ni matokeo ya kampeni hii ambayo kimsingi mkakati wake haulengi faida za kimasoko pekee, bali pia inaunga mkono jitihada za serikali kukuza sekta hii muhimu na zaidi inalenga kumkomboa mkulima.

"Wito wangu kwa wakulima wa korosho Mkoa wa Mtwara na Lindi tuendelee kuwaunga mkono ndugu zetu hawa kwenye hili.

"Msisitizo wangu kwa wakulima unaendelea kuwa kwenye suala zima la nidhamu ya fedha wanazopata wazitumie vyema. Mafunzo yanayotolewa na benki hii kuhusu umuhimu wa kujiwekea akiba, matumizi ya bima mbalimbali ikiwamo bima ya afya na kuwekeza kwenye zana za kisasa za kilimo," alisema Kanali Abbas. Mkurugenzi wa Idara ya Wateja Wadogo wa Wakubwa wa benki hiyo, Elibariki Masuke, alisema msimu wa tatu wa kampeni hiyo ya miezi mitatu ni mwendelezo wa mkakati wa benki hiyo wa kuitikia wito wa serikali kuchangia katika kufanikisha ajenda 10/30 ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo kutoka asilimia tano hadi 10 ifikapo mwaka 2030.

Alisema kuwa kupitia kampeni hiyo, wanatoa zawadi kwa wakulima ili kuongeza motisha na ufanisi wao katika uzalishaji mashambani.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Mtwara-Mikindani, Shadida Ndile na Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Mtwara, Kakozi Ibrahimu walionyesha kuguswa na kampeni hiyo.

Walisema inawasaidia wakulima ambao awali licha ya kupata fedha nyingi kupitia mauzo ya korosho, hazikuwasaidia kujikwamua na umaskini.

Mnamo Agosti 18 mwaka huu, jijini Tanga, aliyekuwa Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde (sasa Waziri wa Madini), alisema dhamira na shabaha ya serikali ni kuhakikisha zao la korosho linachangia kuongeza ajira na kipato kwa wakulima kupitia uongezaji thamani.

Alibainisha kuwa zao la korosho pamoja na kuendelea kuwanufaisha wakulima, pia linaoongoza kwa kuliingizia taifa fedha za kigeni ambapo kwa msimu uliopita wa mwaka 2022/23 liliingiza Dola za Marekani milioni 226.9.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA YA DAR ES SALAAM
SHAURI LA MAOMBI NAMBA 548 YA MWAKA 2023
IRENE RICHARD SUMA..........................MUOMBAJI
DHIDI YA
ERIC RICHARD SUMA
(Personal Legal Representative of RICHARD SUMA)...........1. MJIBU MAOMBI
ERIC RICHARD SUMA.......................................................2. MJIBU MAOMBI
DPI SIMBA LIMITED.......................................3. MJIBU MAOMBI
EXCESS CONSTRUCTION COMPANY LIMITED.........................4. MJIBU MAOMBI
JESCA W.L. MASSAWE T/A
JJ AUCTION MART LIMITED.......................................5. MJIBU MAOMBI

KWA: JESCA W.L. MASSAWE
T/A JJ AUCTION MART LIMITED
SIMU:0718492834
DAR ES SALAAM.

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa muombaji aliyetajwa hapo juu amefungua shauri dhidi yenu, shauri ambalo maelezo yake yameelezwa katika nakala za hati ya madai zinazopatikana katika Mahakama hii, mnatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii, nyinyi wenyewe au wakili au mwakilishi wenu ambaye anaruhusiwa kisheria siku ya tarehe 9/10/2013 saa mbili (2:00) asubuhi mbele ya Mhe. E.E. KAKOLAKI, J kujibu madai hayo dhidi yako. Mnaagizwa kuleta vielelezo vyote mnatarajia kuvitumia katika utetezi wenu siku hiyo.

**ANGALIAI** Kama msipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikathibitisha kuwa mmepokea taarifa hii ya shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wako.

HATI hii imetolewa kwa MKONO wangu na CHAPA ya Mahakama leo hii tarehe 5 mwezi wa 10 Mwaka 2013.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU



Lindi Jumbo Limited

VACANCIES

**About Lindi Jumbo Ltd**

Lindi Jumbo is a Tanzanian graphite mining company developing a high-grade, low-cost mine expected to begin production in early 2024. The company is well-positioned to capitalize on the growing demand for graphite as the world transitions to a clean energy economy. Lindi Jumbo is committed to sustainable mining practices and contributing to the social and economic development of the Lindi Region.

- Technical Services Manager
- Metallurgist x3
- Cost/Management Accountant
- Supply Chain & Contracts Superintendent
- HSE Superintendent
- Procurement Officer
- Logistics Officer
- Safety Officer
- Environmental Officer
- Engineering Foreman
- HR Officer
- HR/Payroll Clerk

➢Location: Matambarale, Ruangwa District, Tanzania.
➢Closing Date: 23rd October 2023, 4:00PM (GMT+3)

To apply or view more details visit: https://jobportunities.net/jobs_search.aspx or scan the QR Code.

*For assistance on the portal, please contact the Lindi Jumbo at +255 22 260 2770.*
*Alternatively send an email via the recruitment portal's Contact Us page.*

217635402

# TRA yabaini stempu bandia, mmiliki wa kampuni akamatwa

**Na Jumanne Juma**

TIMU maalum ya ukaguzi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imebaini kuwapo stempu za ushuru za kughushi zinazobandikwa katika bidhaa.

Meneja wa TRA Mkoa wa Arusha, Eva Raphael, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa baada ya timu hiyo kufanya ukaguzi katika Kampuni ya Double Diamond Holdings ya mkoani mwake, imebaini stempu ambazo hazijatolewa na TRA.

Alisema walifanya ukaguzi wa kawaida wa kuwatembelea wazalishaji bidhaa hizo katika kampuni hiyo na kukuta katoni zaidi ya 600 zimebandikwa stempu za ushuru na lora moja la stempu zinazodhaniwa za kughushi kutoka katika kampuni hiyo.

Alisema kuwa katika kampuni hiyo inayojihusisha na uzalishaji pombe kali, wamebaini kuwapo zaidi ya katoni 900 zilizozalishwa muda mrefu, lakini hazikubandikwa stempu. "Timu hii maalum imefanya ukaguzi wa kawaida katika kampuni hii na tumebaini kuwapo stempu hizo za ushuru zinazodhaniwa za kughushi na lora moja, ni hatari sana kwa afya za watumiaji wa bidhaa hizo," alisema.

Eva alisema mmiliki wa kampuni hiyo ameshafikishwa katika vyombo vya usalama kwa hatua zaidi za kisheria.

Pia aliwaasa wazalishaji wengine kuacha kughushi kwa kuwa ni hatari kwa afya za watumiaji wa bidhaa zao, pia kunasababisha upotevu mapato ya serikali, jambo ambalo ni uhujumu uchumi.

"Rais Samia Suluhu Hassan anapambana ili wananchi wawe na maisha mazuri, wapate huduma bora za kijamii, vyote vinatokana na kodi zetu tunazolipa. Kwahiyo, tuwe wazalendo kwa kulipa kodi," alisisitiza.

Aliwataka wazalishaji kuwa wazalendo wa kufuata sheria zinazowaongoza kutekeleza majukumu yao ya uzalishaji bidhaa zao ili kuepuka usumbufu.

Pia aliwataka wananchi kuhakiki bidhaa za vinywaji kwa kutumia Hakiki App kabla ya kutumia bidhaa hizo kwa manufaa yao.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (kulia), akipokea Mwenge wa Uhuru jana kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rose Senyamule, ambao utakagua, kuzindua na kuweka jiwe la msingi kwenye miradi 58 ya thamani ya Sh. bilioni 13.2 katika Kata ya Dosidosi wilayani Kiteto. **PICHA: GIFT THADEY**

# Meli mpya kujengwa Tanganyika

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imesema itajenga meli mpya ya mizigo baada ya kukamilika kwa ujenzi wa Bandari ya Karema, Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi.

Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alisema hayo alipotembelea bandari hiyo wakati wa ziara ya kukagua miradi ya maendeleo.

Alisema watajenga barabara ya kiwango cha lami na reli ili kuwezesha bandari hiyo kufanya kazi kwa uwezo wake.

"Nimefurahi kuona bandari hii yenye miundombinu ya kisasa na nafasi ya kutoa huduma bora za kibandari kwa wananchi na wafanyabiashara wa ndani na nchi jirani ikiwamo Zambia na Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC)," alisema Mbarawa na kuongeza;

"Tutajenga meli hiyo ili uwekezaji wa serikali wa Sh. bilioni 47.9 uweze kuleta tija ni lazima ipatikane meli kubwa ya mizigo sambamba na ujenzi wa barabara ya lami na reli kilomita 110 kutoka Mpanda hadi Karema."

Mbunge wa Mpanda vijijini na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Moshi Kakoso, alisema wananchi wa mikoa ya Katavi, Rukwa na Kigoma wanamshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa mradi mkubwa wa bandari ya kimkakati ya Karema ambayo itainua uchumi wa mikoa hiyo kwa kiasi kikubwa na kutoa fursa za ajira kwa wananchi.

Meneja wa Bandari za Ziwa Tanganyika, Edward Mabula, alisema tangu kuanza kutumika kwa Bandari ya Karema, Septemba Mosi, 2022, imehudumia abiria 4,900 na tani 1,500 za mizigo zimesafirishwa kupitia bandari hiyo.

Alisema Oktoba 11, mwaka huu, serikali inatarajia kutia saini mikataba ya ujenzi wa meli mbili za mizigo zitakazotoa huduma katika Ziwa Victoria na Tanganyika sambamba na mkataba wa ujenzi wa karakana ya meli na hafla ya utiaji saini huo inatarajia kufanyika mkoani Kigoma.

## Mkakati kuingiza Tanzania uchumi dijitali kuimarishwa

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

TANZANIA haitaweza kuingia kwenye uchumi wa kidijitali bila kuwa na miundombinu ya utambuzi kwasababu unajumuisha ufikishaji wa barua, vipeto na huduma nyingine za nyumbani zinazoweza kufanyika kupitia anwani za makazi.

Mratibu wa Utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi nchini, Jampion Mbugi, alisema hayo mjini hapa wakati wa ufunguzi wa mafunzo kuhusu utekelezaji wa mfumo huo katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro yalitolewa kwa watendaji kata, wenyeviti wa serikali za mitaa, watendaji wa mitaa na wakusanyaji taarifa zaidi ya 1,200.

Wadau hao wanatarajiwa kufanya uhakiki wa anwani za makazi kwa siku 14 katika maeneo yote ya Manispaa ya Morogoro.

Mbugi alisema Tanzania ina fursa ya kuingia kwenye uchumi wa kidijitali na nchi kunufaika na masuala mbalimbali ya ufikishaji wa huduma kwa urahisi kwasababu mfumo huo umefanikiwa kwa asilimia zaidi ya 95 wakati nchi nyingine za Afrika utekelezaji wake umefikia asilimia kati ya tatu hadi 15.

Alisema kila nchi imeweka mfumo wa utambuzi kulingana na malengo yake na kwa Tanzania umejumuisha masuala mbalimbali yakiwamo ya usalama, ulinzi na biashara mtandao na mafanikio yalitokana na kitendo cha Rais Samia Suluhu Hassan kufanya jambo hilo kuanzia ngazi za wajumbe wa shina.

"Ili mfumo uwe endelevu suala la kujenga uwezo linatakiwa kuwa endelevu kwa kujenga uelewa na kufanya uhamasishaji zaidi, kumekuwa na watu wachache ambao wamejaribu kuthubutu kuharibu miundombinu ya makazi na mingine, lakini sheria zipo na zinatumika kulinda miundombinu hiyo," alisema Mbugi.

Aidha, utekelezaji wa anwani za makazi umefikia asilimia 95 na kuifanya Tanzania kuwa kinara kwa Bara la Afrika, ikilinganishwa na nchi nyingine tangu kuanza kwake 2010.

Alisema, mwaka 2021 utekelezaji ulikuwa asilimia tatu na nchi nyingine Afrika ulikuwa wa kusuasua, lakini kwavile suala hilo ni mtambuka linahitaji ushirikishwaji wa wadau mbalimbali kwavile bado ni mfumo mgumu kwa sababu kila nyumba, mtaa, na barabara zinapaswa kufikiwa.

Ofisa Tawala Wilaya ya Morogoro, Hillary Sagala, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa wilaya aliitaka jamii kutoharibu alama za anwani za makazi, kutokana na baadhi ya maeneo kuondolewa.

"Serikali itaendelea kutoa elimu ya kuongeza uelewa kwa jamii namna ya kuthamini miundombinu hii ambayo imetumia kiasi kikubwa cha fedha kukamilika utekelezaji wake," alisema Sagala.

Mwakilishi wa Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro ambaye ni Ofisa TEHAMA wa Mkoa, Herman Njelekela, alisema mkoa utachukua hatua kwa mtu au kikundi chochote kitakachokwamisha kazi hiyo na kuwataka wananchi wote kuithamini.

# Umeme wa ratiba ulivyogeuka shubiri kwa mafundi seremala

**Na Mwandishi wetu**

UMEME wa ratiba ni kilio kinachosikika katika mikoa mingi nchini. Uzalishaji umepungua katika vyanzo vya nishati hiyo vya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO). Ndicho kilichotangazwa na mamlaka za serikali.

Katika baadhi ya viwanda vidogo vya maseremala mtaani, sasa ni kawaida kuwakuta mafundi hao wakigombana na wateja wao kutokana na kuwachelewesha kukamilisha utengenezaji samani. Umeme wa ratiba si rafiki kwa kazi yao.

Mwishoni mwa wiki, mwandishi wa habari hizi, alishuhudia katika Mtaa wa Umoja Road, Tabata jijini Dar es Salaam, ugomvi uliochukua takribani robo saa kati ya seremala na mteja wake kutokana na fundi kushindwa kutimiza ahadi ya kumpatia kabati lake mwanzoni mwa juma lililopita.

Amina Rajab aliyekuwa katika ugomvi na seremala, alidai alimlipa fundi huyo Sh. 250,000 amtengenezee kabati dogo la milango miwili.

Makubaliano yalikuwa angekabidhiwa kabati Jumanne iliyopita, lakini siku hiyo alipopiga simu kwa seremala, mrejesho ni kwamba alikuwa hajakamilisha kazi kutokana na changamoto ya umeme wa ratiba. Akaahidiwa aende Ijumaa, yaani siku tatu baadaye.

"Huyu dada ni kweli nilimwahidi kumpa kabati lake leo (Ijumaa iliyopita), lakini imeshindikana kwa sababu jana (Alhamisi) hatukuwa na umeme. Kutokana na kukatwa kwa umeme, kazi nyingi zinalala, nimemwambia awe na subira nimalizie kupaka rangi kesho (Jumamosi) nimpe," alijitetea fundi Godfrey Shayo.

Shayo alidai kuwa tangu kuwe na utaratibu wa umeme wa ratiba, imekuwa kawaida kwake kugombana na wateja. Kasi ya utendaji imepungua kwa kuwa wanategemea umeme kwa kiasi kikubwa huku baadhi ya wateja hawana subira.

Anasema kwa sasa wanalazimika kufanya kazi hadi saa sita usiku ili kufidia muda wanaopoteza mchana wakingonja ratiba ya kuwa na umeme, ili kuwaridhisha wateja wao ambao hawajazoea kucheleweshewa huduma.

Fundi wa mageti, Ramadhani Mtemvu, mwenye kiwanda kidogo Kinondoni, mkoani Dar es Salaam, alisimulia kukumbwa na mkasa kama wa Shayo aliposhindwa kutimiza ahadi ya kukamilisha geti la mteja ndani ya wiki mbili. Baada ya mvutano mkali, alilazimika kurudisha fedha kwa mteja.

Alisema kwa kawaida hukamilisha kutengeneza geti dogo ndani ya wiki moja na nusu, lakini tangu umeme uwe wa ratiba, anashindwa kufanya hivyo kwa kuwa nguvu kazi inapungua na kulazimika kutumia wiki mbili.

"Yule dada mara ya kwanza alikuja, nikamwambia 'njoo wiki ijayo', akaja wiki iliyopita nikawa sijalipiga rangi, akasema anataka pesa yake. Bahati nzuri nilikuwa na pesa ya mteja mwingine alikuja kuweka oda siku hiyo. Ikabidi nimpe Sh. 300,000 yake," alidai Mtemvu.

Alilalamika anashindwa kufanya kazi usiku kwa kuwa anaishi Kibaha kwa Mathiasi, mkoani Pwani (umbali wa Km 35.5). Anahofia usalama wake kurejea nyumbani usiku wa manani.

Seremala mwingine kutoka Temeke, Dar es Salaam, Kelvin Kijazi aliwaomba wananchi, hususani wateja wa bidhaa zao, wawe na uvumilivu kipindi hiki ambacho kazi zao zimekumbana na kikwazo cha umeme wa ratiba.

"Tunawaomba wateja wetu watuelewe, hali ndio kama hii imetokea na ipo nje ya uwezo wetu. Sisi wenyewe tunatamani tumalizane na mteja haraka ili kesho arudi tena kwetu," alisema Kijazi.

Ni hoja iliyoungwa mkono na fundi cherehani mwenye ofisi yake maeneo ya Mwenge, Kinondoni, Suzan Alphonce, akiwa na ufafanuzi kwamba mafundi wengi kwa sasa wanatumia cherehani za umeme ili kurahisisha utendaji kazi wao, hivyo nao "wamevurugwa" na umeme wa ratiba.

"Kuna wale ambao wana cherehani mbili - za umeme na kawaida, hawana shida sana. Sasa mimi nina moja tu ya umeme, siku kama ya leo umeme umekatika ndio kama hivi unaniona ninashona viraka kwa mkono," alisema.

Mnamo Oktoba 2 mwaka huu, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Gissima Nyamo-Hanga, akizungumzia hali ya uzalishaji umeme nchini, alisema kuna upungufu wa megawati 300 hadi 350 kutoka 400 za wiki moja nyuma.

Alisema TANESCO ilifanya kazi kubwa ya kutengeneza mitambo na kupata gesi kwa ajili ya kuzalisha umeme zaidi ili kuondokana na upungufu wa megawati 400 katika Gridi ya Taifa.

Siku hiyo, Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, alilielekeza shirika kuharakisha urekebishaji mitambo ili kuimarisha upatikanaji umeme kwa kuwa uzalishaji ukiwa mdogo wakati mahitaji ni makubwa, upungufu wa nishati hiyo unatokea.

Pia aliliagiza shirika kufanyia kazi haraka hitilafu zote zilizotokea ili umeme uendelee kupatikana na kuboresha kitengo cha huduma kwa wateja; wananchi wanapopata hitilafu ndogo za umeme wazitatue kwa wakati.


## Bank of India (Tanzania) Ltd.

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

*Relationships beyond banking*

**ISCLOSURES MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014 AND CONSUMER PROTECTION REGULATION, 2019**
**MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)**

**Service Charges (Exclusive of VAT and Government Levy on DigitalTransactions) (The applicable VAT (Value added Tax) and Govt Levy on digital Transaction to be collected during the collection of service charges)**

A. REMITTANCE –OUTWARD

| Sr. No. | Item | Charge |
|---|---|---|
| **TISS Remittance** (Only for A/c holders – Not permitted for non a/c holders) | Remittance -TZS | TZS 10,000 |
| | Remittance -USD | USD 10 |
| **Other Outward Remittance** | 1USD up to 6,000 | USD 15 |
| | USD 6,001 – 10,000 | USD 30 |
| | Above USD10,000 | @ 0.35% Maximum USD 75 |
| Tracer Charges | Irrespective of Amount | USD 30 |
| Recall back funds charges | Irrespective of Amount | USD 30 |

B. REMITTANCE –INWARD

| Sr. No. | Item | Charge |
|---|---|---|
| (Only for A/c holders – Not permitted for non a/c holders) | From inside Tanzania | Free |
| | From outside Tanzania: as under | |
| | For Current /Overdraft Accounts | 0.35% of inwards remittance Minimum USD 18 Maximum USD 70. |
| | For Saving Accounts | |
| | USD 0 up to USD 100 | Free |
| | USD 101 up to USD 500 | USD 10 |
| | Above USD 500 | USD 18 |

C. DEPOSIT AND RELATED SERVICES

| Item | TZS A/c | USD A/c |
|---|---|---|
| **Saving Account :-** | | |
| Cash withdrawal per day –Free of charge, up to amount | TZS 25 Mn | USD 2000 |
| Cash withdrawal charges over USD 2,000 to USD 5000 per day | -- | 0.25% of withdraw amount |
| Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | -- | 0.60% of withdraw amount |
| Cash withdrawal charges over TZS 25 Mn per day | 0.10% of withdrawal amount | |
| Cash Deposit charges over USD 5,000 per day | -- | 0.60% of deposited amount |
| Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both for below and above USD 5,000) | -- | 12% (Min USD 1) of the aggregate small currency amount |
| **Current Account:-** | | |
| Cash withdrawal per day –Free of charge, up to amount | TZS 25 Mn | USD 5000 |
| Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | -- | 0.60% of withdrawal amount |
| Cash withdrawal charges over TZS 25.00 Mn per day | 0.15% of withdrawal amount | -- |
| Cash deposit charges over USD 10,000 per day | | 0.60% of deposit |
| **Maintenance of minimum balance: -** | | |
| For Saving Account-Without Cheque Book Facility | TZS 50,000 | USD 50 |
| With Cheque Book Facility | TZS 200,000 | USD 200 |
| For Current Account | TZS 200,000 | USD 200 |
| **Minimum balance charges (in case of non-maintenance of minimum balance)** | | |
| Saving Account - Without cheque book | TZS 900 p.m | USD 4 p.m |
| With cheque book | TZS 3600 pm | USD 15 p.m |
| Current Account- | TZS 20,000 p.m | USD 15 p.m |

D. Other Common Charges

| Item | Charges TZS A/c | Charges USD A/c |
|---|---|---|
| Stop Payment Instructions | TZS 35,000 | USD 28 |
| Regular statement of a/c (Monthly) | Free | Free |
| Interim/additional statement | TZS 1500 per page | USD 1.50 per page |
| Issue of bankers' cheque | TZS 40,000 | USD 30 |
| Cancellation of bankers cheque/DD | TZS 20,000 | USD 15 |
| Issue of Duplicate Bankers cheque/Demand Draft/ Duplicate FDR | TZS 30,000 | USD 20 |
| Application charge for Treasury Bond | TZS 100,000 | USD Equivalent to TZS 100,000 |
| Issue of Balance certificate (Saving Account) | TZS 20,000 | USD Equivalent to TZS 20,000 |
| Issue of Balance certificate (Current Account) | TZS 50,000 | USD Equivalent to TZS 50,000 |
| Signature verification and Photo Attestation charges for Domestic A/c Holders | TZS 10,000 | USD Equivalent to TZS 10,000 |
| Verification of Documents such as KYC Documents along with verification of Photo and Signature of Customer Mentioned account with Bank of India- in India /Overseas | TZS 25,000 | USD Equivalent to TZS 25,000 |
| Savings bank customer Identification card- One time | TZS 20,000 | USD 10 |
| Dormant a/c Activation Per Activation Fees | Individual TZS 5,000 Corporate TZS 12,000 | Individual USD 3 Corporate USD 6 |
| Account Freezing/un freezing Charges | Free | Free |
| SMS Alert facility | Free | Free |
| Email Alert Facility | Free | Free |
| Monthly Statement on Registered Email | Free | Free |
| Balance Inquiry (Over the Counter) | Free | Free |
| Charges for Deletion of Decease Person Name from the Saving Account | Free | Free |
| Charges for Addition/modification Account such as Change in respect of Corporate A/c | TZS 20,000 | USD 10 |
| Updating of Mobile No. in A/c (SB,CD,OD) | Free | Free |
| Change /Modification in Address (SB,CD,OD) | Free | Free |
| Issuance of No Dues Certificate for Non-Borrowers. | TZS 10,000 | USD 7 |
| Ledger Folio Charges per Folio (40 lines per Folio) only for Current and Overdraft Accounts | TZS 6,000 per Folio | USD 4 per Folio |
| Postages/Courier Charges Inland/Foreign | TZS 30,000 or actual charges whichever is higher | USD Equivalent to TZS 30,000 |

E. CLEARING SERVICES

| Item | Charge/Fees TZS A/c | Charge/Fees USD A/c |
|---|---|---|
| Within walking distance-1 km | TZS 70,000 | USD 45 |
| Far off distance –more than 1 km | TZS 95,000 | USD 65 |
| Cheque returned charges – financial reasons (inward/outward) | TZS 70,000 | USD 55 |
| Inward/outward cheque collection -USD | 0.60% Min comm.18 postages 90 | 0.60% Min comm.18 postages 90 |

CREDIT MATTERS

| | Charge/Fees |
|---|---|
| **Proposal Processing Charges: -** | |
| New Overdraft/Term Loan/Demand Loan | 1.50% of sanctioned limit (Regular Limit – 1.50% for 12 Months) |
| TOD/TOL/ADHOC | Proportionate to 1.50% for TOL/TOD/ADHOC Period minimum USD 60 |
| New NFB BG/LC Facility | 1.50% of sanctioned limit (Regular Limit – 1.50% for 12 Months) |
| Review of Overdraft Limit | 1.50% on entire sanctioned amount. |
| Review of Term Loan Demand Loan Personal Loan Vehicle Loan Loan Against Property Etc. | 0.15% maximum USD 600 or TZS 1.20Mn on the reviewed amount and 1.50% on the additional Term Loan /Demand Loan amount. |
| Schematic Lending up to 36 months/Staff Loan | Nil |
| Prepayment charges | 2.50% of the prepaid loan amount. |
| Documentation charges for New Overdraft Limit/Term Loan/Demand Loan/Non Fund base Limit | Actuals as per advocate Bill + 0.30% handling charges<br>1) No Documents charges would be applicable for TOD/TOL/ADHOC Limit, however actual expenses if any to be recovered.<br>2) Documentation charges also NOT Recoverable for the Loan/Overdraft against FDR. |
| Charges for Amendments/Modification of Sanction Terms | 0.25% on the sanctioned limit<br>**We enumerate the illustrative instances of Modification in Terms and Conditions to be effected at the request of the Borrower where this charge will be levied: -**<br>1) Substitution of Collateral Securities/Personal Guarantee<br>2) Release of Personal Guarantee/Collateral Security.<br>3) Interchangeability of limits.<br>4) Change in project/items of Machinery<br>5) Ceding of charges on assets(Pari-Passu)<br>6) Restructuring, Rephasement of Loans/ Deferment of Loan installments.<br>7) Approvals for mergers & amalgamations.<br>8) Any other miscellaneous credit related approvals. |
| Revalidation of Sanction | **25% of Applicable PPC Charges on Overdraft Limit/Term Loan/Demand Loan** |
| Lead bank Charges | **USD 1000 or equivalent in TZS per annum/one time** |
| Fee for Opening Escrow/TRA A/cs (Trust and Retention A/cs) | **Where**<br>**We are Lead bank: Nil**<br>**We are Not Lead Bank:**<br>USD 500 or equivalent in TZS per annum/one time |
| Charges for Supplying copies of Loaning Documents to Customer. | First instance: Free<br>**USD 10 or equivalent in TZS for further requirement.** |
| Non/Delayed Submission of Audited Financial Statements of the Company OR wherever applicable | **USD 100 or equivalent in TZS per month or part thereof**<br>**Note:-**Audited Financial statements of the firm/company within 6 months from closure of Financial Year or as approved by TRA for the relevant year. |
| Inspection charge | TZS 30,000 per visit/inspection or at least once in quarter whichever is higher. / TZS 50,000 or equivalent to USD per visit /inspection or at least once in quarter whichever is higher.<br>**Note:-**<br>1) Out of Pocket Expenses to be recovered additionally along with regular inspection charges wherever applicable<br>2) **Project Monitoring Inspection Charges/Technical Due Diligence Inspection charges:** Considering the fact that this inspection is proposed for safeguarding banks Interest, normal inspection charges besides travelling, boarding/lodging expenses are to be recovered from the borrower. |

| | | |
|---|---|---|
| Issuance of No objection certificate (NOC) | **USD 100 or equivalent in TZS** | |
| 1st party/3rd party Overdraft/Loan against deposit of our Bank (BOITL) | Waiver of Processing & Documentation charge. | |
| Overdraft/Term Loan/Demand Loan Conversion Charges (Currency Conversion) | For Overdraft account 0.50% of Sanction Limit.<br>For Term Loan/Demand Loan 0.50% of O/s Amount | |
| Earmarking of Limits | **USD 500 or equivalent in TZS per annum** | |
| Non Compliance of Sanction terms/Commitment charges | **1.00% additional Penal Interest to be charge till compliance of Sanction terms** | |
| **D&B/ Other Credit Information Search for per Borrowal a/c (New/Additional/Review of limit)** | | |
| | USD Facility | TZS Facility |
| Up to TZS 20 Mn/USD 10,000 (Only for new and additional Limit. **Review – No charge**) | USD 5 | TZS 5,000 |
| Over USD 10,000 to USD 50,000/ Over TZS 20 Mn up to TZS 100 Mn | USD 10 | TZS 20,000 |
| Over USD 50,000/TZS 100 Mn | USD 50 | TZS 100,000 |
| D&B Search for non-Borrower, on request | USD 50 | TZS 100,000 |
| Charges for Furnishing copy of Credit Information report obtained from CIC | **TZS 20,000** | **USD 10** |
| **Guarantee (Performance/Financial) :-** | | |
| Guarantee Commission | 1.35% per quarter or part thereof minimum for one quarter. | |
| Guarantee against 100% cash margin | 50% concession on the above rate | |
| Swift Charges | **As Applicable** | |
| Postages | **As Applicable** | |
| Revert of Guarantee before Expiry | **Minimum 1 Qtr BG Commission to be recovered for part of quantum of full guarantee commission to be recovered** | |
| Closure of Guarantee After Expiry of Claim Period | Nil | |
| Invoke of Guarantee | **USD 200 or equivalent in TZS** | |
| | **A. Financial Guarantees: -**<br>1. In favour of Customs/Excise/Tax Authorities towards tax/Duties payment Etc.<br>2. Favouring Courts for Release of Amounts.<br>3. For Guaranteeing Loan payments.<br>**B. Performance Guarantees: -**<br>1. In lieu of earnest money deposit<br>2. In lieu of tender deposit<br>3. In lieu of security deposit<br>4. To obtain advance payments (generally exports)<br>5. To obtain mobilization advance (generally domestic)<br>6. Towards Direct/indirect taxes to govt. in respect of specific transaction.<br>7. For Direct/indirect taxes disputes with tax Authorities.<br>8. For payment for supplies/services made /rendered<br>9. For Securing retention amount<br>10. For Bidding/tendering for Project Contacts<br>11. For Performance in terms of any agreed contact.<br>**Note: - No processing charges or documentation charges are to be levied in case of Casual BG limits issued against 100% or more cash margin.** | |
| **Imports :-** | | |
| LC Opening charges | 1.35% per quarter +SWIFT charges USD 30/- | 1.35% per quarter +SWIFT charges USD 75/- |
| Against 100% cash margin | 50% concession on the above rate i.e. 0.67% per quarter +SWIFT charges USD 30/- | 50% concession on the above rate i.e. 0.67% per quarter +SWIFT charges USD 75/- |
| LC Amendment Charges | Per amendment 0.40% of LC amount (minimum USD 60 and Maximum USD 325) +SWIFT charges USD 30 (Same for LC against 100% cash margin) | |
| Acceptance of bills under LC | 0.60% of Bill amount Min USD 30 Maximum USD 180 | |
| Retirement of bills under LC | 0.60% of Bill amount Min USD 30 Maximum USD 360 | |
| Inward Bills for Collection | 0.30% of Bill amount minimum USD 150 | |
| **Exports:-** | | |
| Negotiation of Bills under LC | 0.60% of Bill amount Minimum USD30 Maximum USD 360 | |
| Confirmation of Export LC | 0.90% per quarter +SWIFT charges USD 30/- | |
| LC Advising Charges | USD 150 | |
| Export Bills for Collection | 0.60% of Bill amount Minimum USD 30 Max USD 360. | |
| Charges for Certifying invoices subsequent to negotiation | **USD 10 Per Invoice** | |
| Clean payment Received under LC | **USD 100 per occasion** | |
| Advice of transfer in transferable LC | **USD 100 per advice of transfer and acceptance commission at 0.30% Minimum USD 100** | |

OTHER DISCLOSURES
(VIAMBATANISHI NYINGINEZO)

| No. | ITEM/TRANSACTION | USD | TSHS |
|---|---|---|---|
| 1.0 | **Base or Prime Lending rate** | 7.50% p.a. | 14.50% p.a. |
| 2.0 | **Maximum Spread above Base or Prime Lending rate** | 7.00% | 7.00% |
| 3.0 | **Penal interest** | | |
| a) | For Non Compliance of Terms of sanction | 3% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| b) | For Overdrawing/ Excess Drawings due to non – payment of interest/ Instalments/ Charges | 5% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| 4.0 | **Deposit Rate** | | |
| i) | Current Deposit | Nil | Nil |
| ii) | Savings Bank Deposit | 0.50% p.a. | 2.50% p.a. |
| iii) | Fixed/Recurring/QIC/MIC deposit | **Up to USD 10,000** | **Up to TZS 10,000,000** |
| | 6 months | 3.00% | 6.25% |
| | Over 6 months | 3.50% | 7.25% |
| | | **Over USD 10,000** | **Over TZS 10,000,000** |
| | 6 months | 3.50% | 6.75% |
| | Over 6 months | 4.00% | 7.75% |
| | * No interest is payable in case of premature withdrawal of fixed deposits | | |

**No Penalties & Other sanctions have been imposed by Bank of Tanzania (BOT)during the Period covered by the Disclosure**

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name. | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Antaryami Sarangi | Managing Director | Signed | 03.10.2023 |
| 2. | Heriabdiel Ayoh | General Manager | Signed | 03.10.2023 |
| 3. | Robert Kibona | General Manager | Signed | 03.10.2023 |

217634502

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga jipangeni sasa, robo fainali CAF inawezekana

**SHIRIKISHO** la Soka barani Afrika (CAF), tayari limepanga makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika na yale ya Kombe la Shirikisho huku likitangaza kati ya Novemba 24 na 25, mwaka huu, ndizo tarehe za mechi za hatua hiyo zitaanza kuchezwa.

Kwa Tanzania inawakilishwa na Simba na Yanga kwenye Ligi ya Mabingwa baada ya Azam FC na Singida Fountain Gate, kuondoshwa katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Katika droo ya makundi iliyochezeshwa Ijumaa iliyopita nchini Afrika Kusini, Simba imepangwa Kundi B pamoja na wanafainali wa michuano hiyo msimu uliopita, Wydad Casablanca ya Morocco, Asec Mimosas ya Ivory Coast na Jwaneng Galaxy ya Botswana.

Kwa upande wa Yanga, ambayo imeingia hatua ya makundi kwa mara ya kwanza baada ya miaka 25, imeangukia Kundi D pamoja na mabingwa watetezi, Al Ahly ya Misri, CR Belouizdad ya Algeria na Medeama ya Ghana.

Kwa ujumla si makundi mepesi na kwa tafsiri nyepesi kundi la Simba nje ya uwanja wengi wanaona nafasi moja ni ya Wydad na moja iliyobaki ni kwa timu nyingine tatu kuingia katika kinyang'anyiro cha kuwania kuungana nayo kwenda robo fainali. Kadhalika katika kundi la Yanga, nje ya uwanja wengi wanaona nafasi moja inatolewa kwa Al Ahly na iliyobaki timu tatu ziigombanie.

Lakini sisi tunaamini pamoja na ukubwa na ukongwe katika michuano hiyo, si Wydad wala Al Ahly, ambayo inaweza kujihakikishia kutinga robo fainali kabla ya kumalizika dakika 540 za mechi zote sita za hatua hiyo ya makundi.

Kama msimu wa 2020/21 kwenye michuano hiyo Simba ikiwa Kundi A pamoja na Al Ahly, AS Vita ya DR Congo na Al Merrikh ya Sudan, ilifanikiwa kuongoza kundi kwa pointi 13, ikifuatiwa na Al Ahly iliyokusanya alama 11, huku zote zikichezea kichapo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, kwa nini isiwezekane msimu huu?

Pia msimu ulioisha tu hatua ya robo fainali, Simba iliichapa Wydad bao 1-0 Uwanja wa Benjamin Mkapa na kwenda kutolewa kwa mikwaju ya penalti nchini Morocco baada ya wenyeji wao nao kushinda 1-0, hilo pia linatupa matumaini kuwa wawakilishi hao wa Tanzania wakijipanga hakuna linaloshindikana. Tuna kila sababu ya kuwapa nafasi ya kutinga robo fainali wawakilishi hao wa nchi kwenye michuano hiyo ya CAF kwa ngazi ya klabu barani Afrika hasa ukizingatia Simba na Yanga zote zimefanya usajili mkubwa na wa kimkakati kwa kuangazia michuano hiyo mikubwa kwa ngazi ya klabu Afrika.

Kikubwa ni klabu hizo kuanza maandalizi makubwa sasa, kwani kuna zaidi ya mwezi wa kujiandaa kabla ya hatua hiyo ya makundi, kwa kumulika maeneo yaliyoonekana kuwa dhaifu wakati zilipokuwa zinawania kufuzu hatua ya makundi lakini kutumia mechi za Ligi Kuu kuboresha kila mapungufu yanapojitokeza.

Tunaamini kama msemo wa Simba wa 'Kwa Mkapa Hatoki Mtu', watautumia vema sambamba na Yanga kwa kugeuza kuwa uwanja wao wa kuvuna alama tatu katika kila mechi ya nyumbani na kwenda angalau kupata pointi mbili ugenini, njia ya robo fainali itakuwa imefunguka kwao.

Tangu mwanzoni mwa msimu Simba iliweka malengo ya kufika nusu fainali huku Yanga malengo yao yakiwa kutinga hatua ya makundi, lengo ambalo tayari limetimia ila sisi tunataka kuona sasa wakitangaza malengo makubwa ili kila mchezaji akishuka dimbani ajue nini klabu inakitaka katika michuano hiyo.

Hayo yakifanyika huku viongozi, mashabiki na wapenzi wa kila klabu hizo wakizingatia kushinda mechi zake na kuacha utamaduni wa kuwabeba wageni wanapokuja kucheza hapa nchini, tunaamini Simba na Yanga kila moja inauwezo wa kupata alama tatu kwa Mkapa na kutinga robo fainali.




Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge



# Wawakilishi wa Tanzania CAF mulikeni haya kuvuka makundi

Na Adam Fungamwango

**IJUMAA** iliyopita tulishuhudia droo ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi ikipangwa nchini Afrika Kusini, huku wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano hiyo, Simba na Yanga, zikipangwa makundi tofauti.

Ni tofauti na mashabiki wengi walivyofikiri awali, au kutaka iwe, timu hizo zipangwe kundi moja. Badala yake ni timu za Tunisia, Etoile du Sahel na Esperance ndizo zilizopangwa kundi moja, hata Al Ahly na Pyramids za Misri nazo zilikwepana.

Mabingwa wa Tanzania Bara, Yanga wakaangukia Kundi D na timu za CR Belouizdad ya Algeria, Medeama ya Ghana na Mabingwa Watetezi, Al Ahly ya Misri, huku Simba wakiwa ikipangwa Kundi B, pamoja na timu za Wydad Casablanca ya Morocco, ASEC Mimosas ya Ivory Coast na Jwaneng Galaxy ya Botswana.

Ukiyatazama makundi hayo yote ni magumu kama ilivyo kwa michuano yenyewe. Kwa kawaida Ligi ya Mabingwa Afrika kuanzia ngazi ya makundi huwa hakuna lelemama. Kuna timu ngumu ambazo zenyewe ngazi hiyo ya makundi, robo, nusu hadi fainali ni kama maskani kwao. Huwa zinacheza maeneo hayo kwa miaka nenda rudi hata kama hazijatwaa ubingwa. Zingine huwa zinatwaa kabisa na ubingwa wenyewe na zipo zinazopokezana.

Unapoingia kwenye hatua hii haipaswi kuiogopa timu yoyote zaidi ya kuajindaa kupambana nayo. Mfano ni Simba ambayo 2019 ilipotinga kwa mara ya kwanza kwenye makundi tangu 2003, ilikuwa kundi moja na Al Ahly na kutandikwa mabao 5-0 ugenini.

Kabla ya hapo ilikuwa imeshakula mabao kama hayo dhidi ya AS Vita Club, lakini ikijitahidi kupambana na mwisho wa siku ilifanikiwa kuvuka kundi hilo.

Lilikuwa kama funzo, kwani 2021, Simba tena ilipangwa na Al Ahly kundi moja, pamoja na kwamba ilikuwa kama mwanzo, ilishinda nyumbani na kufungwa ugenini lakini haikuruhusu mabao 5-0, ilifungwa bao 1-0 na ndiyo mwaka ambao iliongoza kundi hilo mbele ya mabingwa hao.

Al Ahly ilihangaika sana kwani ilikuwa almanusura ikose nafasi ya kwenda robo fainali mbele ya AS Vita Club kwani timu hizo ndizo zilibaki zinagombania nafasi moja iliyobaki, Simba ikijihakikishia mapema.

Huu ni mfano ambao unaweza kutumiwa na Yanga kwenye kundi hilo ili kujihakikisha kutinga hatua ya robo fainali. Haipaswi kuhofia sana kwani hakuna jinsi ya kukutana na wababe wa aina hiyo kwenye hatua hii.

Nadhani kwa upande wa Simba imeshakuwa sugu kukutana na timu za aina hii, miezi sita tu iliyopita ilikutana na Wydad Casablaca kwenye hatua ya robo fainali na kutolewa kwa mikwaju ya penalti.

Kinachotakiwa kwa sasa ni kufanya maboresho madogo ya vikosi vyao kwenye mapungufu yanayoonekana wazi kabla ya kucheza hatua hiyo kuna dirisha la usajili kwa ajili ya kuvifanyia vikosi marekebisho. Kwa upande wa Yanga wanaonekana hawana straika mwenye kariba ya Fiston Mayele aliyetimkia Pyramids ya Misri.

Wanapaswa kuingia sokoni kusaka mpachika mabao kabla ya kuanza kampeni ya kwenda robo fainali, vinginevyo itakuwa kwenye maisha magumu mno.

Simba inapaswa kutafuta kiungo mkabaji asilia wa kiwango cha juu na mpambanaji, pamoja na beki mmoja ambaye anaweza kucheza kushoto na kulia anayeaminika, ili kuwasaidia Shomari Kapombe na Mohamed Hussein 'Tshabalala', tofauti na Israel Mwenda na David Kameta ambao hata kwenye Ligi Kuu tu hawaaminiki.

Mechi dhidi ya Power Dynamos imeonesha kuwa tayari wapinzani wengi wameshaisoma na kugundua upenyo unaweza kuwa pembeni, ndiyo maana Joshua Mutale aliwasumbua sana kina Kapombe na Tshabalala, ikionekana ni maagizo ya kocha wake baada ya kuyafanyia kazi mapungufu ya wapinzani wake.

Simba ina tatizo ikiwa haina mpira, na mabeki wake wanafikiwa kwa urahisi sana pale wapinzani wanapojibu shambulizi.

Kwa sasa inakosa kiungo mkabaji asilia kama ilivyokuwa na Gerson Fraga, James Kotei, na Thadeo Lwanga. Kama ikipata kiungo wa aina hii tu naiona ikivuka makundi na kufanikiwa kucheza hata nusu fainali ambayo ni malengo yao makubwa msimu huu kwenye michuano hiyo.

## HABARI KITAIFA

# Biteko azindua mpango kutangaza vivutio vya utalii

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amezindua mpango mkakati wa kutangaza fursa za Sekta ya Utalii katika Wilaya ya Pangani, mkoani Tanga, ili kuunga mkono jitihada za Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika kuikuza sekta hiyo nchini.

Dk. Biteko alizindua mpango huo juzi jijini Dar es Salaam katika kongamano la Uwekezaji la Swahili International Tourism Expo lenye lengo la kutangaza fursa za uwekezaji katika wilaya hiyo ikiwamo utalii katika mbuga ya Saadani, fukwe, kilimo biashara pamoja na uchumi wa Buluu katika wilaya hiyo.

Vile vile, alisisitiza kuwa kongamano hilo litumike kuitangaza Wilaya ya Pangani na kubadilishana mawasiliano ili fursa zilizoko Pangani ambazo hazipatikani kwengine zishawishi watu wengine kuzifuata.

"Niwapongeze sana watu wa Pangani kupitia Mkuu wa Wilaya kwa ubunifu huu wa hali ya juu na nitoe wito kwa wilaya zingine kuiga Pangani na kufungua fursa za utalii na uwekezaji kwenye wilaya zao," alisema Dk. Biteko.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Dunstan Kitandula, alisema, sekta ya utalii kwa sasa mchango wake katika Pato la Taifa ni asilimia 17. Alisema serikali itaendelea kuboresha mazingira rafiki katika sekta hiyo ili kuvutia utalii nchini katika maeneo mbalimbali hususan Wilaya ya Pangani.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Pangani, Zainabu Abdallah, alisema, Wilaya ya Pangani imejikita kwenye uwekezaji wa maeneo matatu ikihusisha utalii, kilimo mkakati na uchumi wa buluu na kuongeza kuwa wilaya hiyo ni miongoni za kimkakati yenye mazingira mazuri ya uwekezaji.

"Serikali imeweka mazingira mazuri ya uwekezaji na tunawaomba wawekezaji kufika Wilaya ya Pangani kujionea fursa hizo muhimu," alisisitiza Zainabu.

Uzinduzi wa mpango huo ulikwenda sambamba na kongamano la uwekezaji chini ya maonyesho ya wadau wa sekta ya utalii kuunga mkono fursa za uwekezaji.

Wengine walioshiriki hafla hiyo ni viongozi mbalimbali wa serikali, watendaji wa taasisi zilizopo chini ya wizara hiyo na wadau wa sekta ndani na nje ya nchi.




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, akipokea tuzo maalumu ya mchango anaoutoa kwenye sekta ya utalii kutoka kwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Dunstan Kitandula, kwenye uzinduzi wa mpango mkakati wa kukuza utalii wilayani Pangani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanahisa NICOL kufaidi gawio la bilioni 2.6/-

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI ya Uwekezaji NICOL, imetangaza kutoa gawio la Sh. bilioni 2.6 kwa wanahisa wake zitakazolipwa mwishoni mwa mwaka huu.

Azimio la kutoa gawio hilo lilifikiwa mwishoni mwa wiki katika mkutano mkuu wa tisa wa wanahisa wa kampuni hiyo uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Mkurugenzi wa NICOL, Erasto Ngamilaga, alisema wanahisa wameazimia gawio hilo lilitolewe kabla ya Desemba 4, mwaka huu.

Alisema kampuni imeendelea kufanya vizuri kwenye soko kwa kuwa mwaka jana ilitoa gawio la Sh. 37 kwa hisa, lakini mwaka huu imeongezeka na kufikia Sh. 43 kutokana na faida ya uwekezaji mzuri walioufanya.

"Tunashirikiana na wanahisa, menejimenti na bodi katika kutekeleza mikakati mbalimbali tuliyonayo na mkakati wa muda mrefu ni kuingia kwenye uwekezaji wa kilimo kwasababu tumeona fursa hiyo," alisema.

Alisema NICOL itatumia fursa ya kilimo kujenga maghala mbalimbali ya bidhaa nchi nzima kutokana na serikali kuweka mazingira mazuri ya kilimo ambacho kitakuwa na faida kubwa.

Pia alisema NICOL imeona fursa za uwekezaji kwenye nishati, madini na gesi na wako kwenye mchakato wa kuanzisha kampuni zitakazohusika na uwekezaji huo.

Mwenyekiti wa Bodi ya NICOL, Dk. Gideon Kaunda, alisema faida waliyopata inatokana na kampuni kuwekeza kwenye miradi mbalimbali yenye tija ambayo imesababisha faida kubwa.

Alisema kwenye mkutano huo wanahisa wamefurahi kutokana na kuongezeka kwa gawio na mwaka huu watalipwa mara mbili ya lililotolewa mwaka jana.

Alisema wamewekeza kwenye hatifungani za serikali na kufanikiwa kupanua shirika kwa kuanzisha kampuni ndogo ya NICOL ya kuwekeza kwenye majengo Real Estate.

"Miongoni mwa mafanikio makubwa ya mwaka jana ni kununua Kampuni ya Mirambo Street Properties Limited kwa hiyo tunatarajia faida itaendelea kuongezeka na mwakani gawio litaongezeka maradufu," alisema Dk. Kaunda.

Alisema hisa za NICOL kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), zimeendelea kupanda na wananchi wengi wameonyesha nia ya kununua hisa ili wawe sehemu ya umiliki wa kampuni.

"Na thamani ya hisa zetu imeendelea kupanda mwaka hadi mwaka, tulianza hisa zetu zikiwa na thamani ya shilingi 270 na sasa zinauzwa shilingi 500 na zitaendelea kupanda kwasababu watu wengi wameonyesha nia ya kutaka kuzinunua," alisema.

Mmoja wa wanahisa mwanzilishi wa NICOL, Alan Mwaigaga, alisema amefurahi kuona kampuni ambayo ameanza nayo miaka mingi iliyopita inazidi kukua.

"Katika siku ambazo nitapata usingizi mwororo ni leo kwa kuona uwekezaji wa NICOL uliotumia akili kubwa nikipita lile jengo la Mirambo na kuona kwamba ni mali yetu najivuna sana na wanahisa wa NICOL watembee kifua mbele popote walipo ule ni uwekezaji wenye akili," alisema.

Mwanahisa Suzana Michael, alisema amefurahi kuona kampuni hiyo inaendelea kupata mafanikio makubwa kwa kuwekeza kwenye miradi mbalimbali ikiwamo ununuzi wa hatifungani za serikali.


**The Guardian Limited**

**VACANCY**

**Freelancer Sales Executive**

**The Guardian Limited** is looking for self driven sales personnel to join our advertising sales team in **Dar es Salaam, Mwanza, Moshi/Kilimanjaro, Arusha, Mbeya, Tanga and Iringa**

**Responsibilities**

- Be responsible for aggressive development of new clients and growing existing business.
- Proactively develop new business avenues
- Devise and monitor business plans to ensure substantive sales
- Develop strategic solutions that meet the unique needs of each client

**Qualifications**

- The position requires someone who can deliver the set targets within deadlines under competitive working environment.
- Applicants need to be highly organized, self-motivated with a positive attitude, and can thrive on setting and reaching new goals.
- Holders of a University degree or Diploma in Business Administration
- Experience in Sales and Marketing is an added advantage

**NOTE: This is a commission Based Position**

**Please send application via Email to vacancy@guardian.co.tz before 15th October, 2023.**



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (wa nne kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Kutengeneza Ndege ya Airplanes African Limited, Leo Minor Tanzania Limited ya mkoani Morogoro, Dk. David Grolig (aliyeinama), wakati wa Maonesho ya Viwanda yaliyofanyika Diamond Jubilee jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali, CTI wapata mbinu kuongeza masoko kimataifa bidhaa za Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema serikali kwa kushirikiana na Shirikisho la Wenye Viwanda nchini (CTI) wataandaa maonesho ya kimataifa ya viwanda mwakani ili kuleta tija kwa wadau wa viwanda na kupata masoko ya kimataifa kwa bidhaa za Tanzania katika nchi mbalimbali.

Dk. Mpango alibainisha hayo wiki iliyopita kupitia hotuba yake iliyosomwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, wakati wa uzinduzi wa maonesho ya viwanda yaliyoandaliwa na CTI kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), jijini Dar es Salaam.

Makamu wa Rais alisema serikali inatambua mchango wa sekta binafsi katika kukuza uchumi na kwa Pato la Taifa. Zaidi ya viwanda 200 kutoka ndani na nje ya nchi vimeshiriki maonesho hayo.

Mkurugenzi Mkuu wa CTI, Leodgar Tenga, alisema wamejipanga mwakani kushirikiana na mabalozi wanaowakilisha nchi zao nchini kushiriki katika maonesho ya viwanda ili kuongeza tija na mafanikio makubwa kwa wadau wa viwanda nchini.

Mwenyekiti wa Bodi ya CTI, Paul Makanza, alisema kuwa kwa mara ya kwanza CTI imeandaa maonesho ya viwanda nchini ambayo yatahusisha wazalishaji wa ndani na nje ya nchi, ikishirikiana na TanTrade.

Alisema lengo la maonesho hayo ni kutangaza bidhaa za viwanda zinazozalishwa ndani na nje ya nchi na kujifunza teknolojia mpya kwa ajili ya kuboresha uzalishaji bidhaa za viwanda.

"CTI imefanikiwa kuwapata wenye viwanda watakaoonesha bidhaa za viwanda kutoka sekta mbalimbali, ikiwa ni pamoja na bidhaa za chuma, kimekali, usindikaji chakula, ujenzi na mashine za viwandani.

"Maonesho haya yanajumuisha magari na ndege zilizoungan-ishwa nchini. Mbali na wenye viwanda, pia zipo taasisi za serikali, balozi na taasisi za sekta binafsi kama TPSF, TCCIA, TWCC na wadau wengine wa sekta ya viwanda ambao jumla yao kwa pamoja wanazidi 200.

"Maonesho ya Kimataifa ya Wazalishaji Tanzania (TIMEXPO) 2023 ni jukwaa la kipekee la kuhimiza na kutangaza ukuaji wa viwanda nchini," alisema.

Akifafanua zaidi kuhusu malengo ya maonesho hayo, Makanza alisema yanajumuisha kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, hivyo kukuza uwekezaji nchini; kutangaza bidhaa na huduma kwa wateja, wawekezaji na wazalishaji kutoka ndani na nje ya nchi na kubadilishana uzoefu na ujuzi wa kiteknolojia na mbinu bora za uzalishaji.

Makanza pia alisema wanalenga kuendeleza ushirikiano wa kibiashara kwa kuwa na uhusiano wa kibiashara wenye manufaa baina ya wazalishaji wa nje na ndani; kuongeza ushindani pale washiriki wanapotathmini bidhaa na huduma zao dhidi ya wenzao na kujifunza jinsi ya kuboresha ubora na ushindani.

"Pia tunalenga kukuza uchumi. Ukuaji wa sekta ya viwanda una athari chanya kwa uchumi wa nchi. Unachangia katika kukuza Pato la Taifa, kupunguza utegemezi kwa bidhaa za nje na kuimarisha upatikanaji na udhibiti wa fedha za kigeni nchini.

"Kwa kuzingatia malengo hayo, tunaweza kusema kuwa Maonesho ya Kimataifa ya Viwanda Tanzania (TIMEXPO) 2023 yatachangia kuchochea maendeleo ya sekta ya viwanda na kukuza uchumi na Tanzania kiujumla.

"Takwimu kutoka kwenye kitabu cha hali ya uchumi 2022, zinaonesha katika mwaka 2022 viwanda nchini vilichangia kwa asilimia 7.1 kwenye Pato la Taifa kulinganishwa na asilimia 7.2 katika mwaka 2021.

"Pia sekta ya viwanda ilikuwa kwa asilimia 4.8 kwa mwaka 2021 kulinganisha na asilimia 4.2 mwaka 2022.

Takwimu hizi zinaonesha kushuka kidogo kwa viashiria vya ukuaji wa sekta ya viwanda kwa mwaka 2022. Hali hii imetokana na changamoto mbalimbali za uchumi duniani, zikiwamo athari za UVIKO-19 na vita kati ya Russia na Ukraine," alisema.

Kwa kutambua hilo, kiongozi huyo alisema ni muhimu kwa wadau wote wa CTI, serikali na sekta binafsi, kuchukua hatua stahiki za kuimarisha viwanda kwa faida ya maendeleo endelevu ya taifa.

Alisema kuwa katika maonesho hayo, watashuhudia mchangayiko wa ubunifu, ujuzi na utaalamu kutoka kwa wazalishaji. Kila banda na kila bidhaa inayooneshwa ina historia yake, juhudi zake na ndoto za kuchangia kwenye maendeleo ya nchi.

"Ni jukumu letu sote kutumia fursa hii kujifunza kutoka kwa wenzetu na kushirikiana ili kuleta mabadiliko chanya.

"Ninapongeza juhudi zinazooneshwa na serikali katika kuboresha mazingira ya biashara nchini ikiwamo uanzishwaji mikakati na sera zenye lengo ya kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya viwanda pamoja na kutoa fursa za kuongeza uhusiano wa kujenga ushirikiano baina ya sekta ya umma na binafsi.

"Maonyesho haya pia ni hatua moja muhimu katika safari hii ya kuelekea uchumi wa viwanda. Sisi CTI jukumu letu kubwa ni kuchagiza mazingira bora ya biashara kwa wazalishaji wetu na kuunga mkono juhudi za serikali katika kuendeleza jambo hili.

"Ninawasihi wenye viwanda na wafanyabiashara kutumia fursa hii kwa ukamilifu. Tuchunguze kwa kina bidhaa na huduma zetu na tuone jinsi tunavyoweza kuziboresha," alishauri.

Mkurugenzi Mkuu wa TanTrade, Latifa Mohammed, alisema lengo la maonesho hayo ni kushirikiana na kuungana kutoa huduma mbalimbali kwa wadau wa viwanda.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alisema serikali itashirikiana na CTI kupata eneo kubwa la wazi ili Watanzania wengi washiriki maonesho hayo na kujifunza teknolojia mbalimbali zinazotumika katika uzalishaji bidhaa na kutoa fursa kwa wenye viwanda kupata masoko ya uhakika.

Akiwakilisha washiriki wa viwanda, Mtendaji Mkuu wa Kiwanda cha Kim kinachozalisha bidhaa za plastiki na mashine za mafuta ya kula cha KOM kilichoko Kahama mkoani Shinyanga, Dk. Joyce Nkwabi, alisema wamekuwa wanatoa huduma kwa jamii na kuhakikisha bidhaa zao zinakuwa na viwango vya kimataifa.

## Pinda 'alia' wakulima kukosa elimu ya matumizi ya mbolea

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, amesema wakulima wengi nchini hawana elimu sahihi ya matumizi ya mbolea wakati wa kilimo ili kuongeza uzalishaji.

Pinda alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipozungumza na walimu wastaafu Mkoa wa Dodoma waliomtembelea shambani kwake eneo la Zinje jijini.

Alisema ili kilimo kiwe na tija na ufanisi, wakulima wanapaswa kuzingatiwa kanuni za kilimo na matumizi ya mbolea ili kuongeza uzalishaji wa mazao wanayolima.

Pinda alisema maofisa ugani nchini wana jukumu la kuwasimamia wakulima kwenye maeneo yao na kutoa elimu kwa wakulima kuhusu ya faida za matumizi ya mbolea.

Alisema wakulima wamekuwa wanajitahidi kuongeza uzalishaji, lakini wanahitaji elimu ili kuongeza tija ya kilimo na kupata mazao ya kutosha.

Vilevile, alisema wananchi wanapaswa kuingia katika ufugaji samaki kwa kuwa shughuli hizo zinahitaji eneo dogo.

Alisema wastaafu ni kundi muhimu katika jamii na wamekuwa na ujuzi tofauti, hivyo wanaweza kusaidia jamii katika fani mbalimbali.

Pinda alisema kuwa iwapo wataungana, watasaidiana kutatua matatizo kutokana na uwezo na ujuzi walionazo kabla ya kustaafu.

Aliwataka wastaafu kujikita katika shughuli za uzalishaji mali hasa kilimo na ufugaji.

Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu Wastaafu Dodoma, Hassan Mbiru, alisema lengo la ziara hiyo ni kujifunza shughuli mbalimbali za kilimo na ufugaji.

"Kwa kweli tumejifunza mengi! Baada ya kustaafu unaweza kufanya shughuli nyingine za maendeleo na kuisaidia jamii," alisema.

Mbiru alisema walikwenda kujifunza kwa Pinda ambaye amejikita katika ufugaji na kilimo kwa mafanikio makubwa.

"Sifa za shamba hilo zimefanya kuwavuta watu wa ndani na nje ya nchi kujifunza," alisema.



# Makinda alipa 'jeuri' Baraza la MoCU utatuzi wa kero

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SPIKA wa zamani wa Bunge, Anna Makinda, amelipa 'jeuri' Baraza la Chuo Kikuu Cha Ushirika Moshi (MoCU), kutokubali kulaza matatizo yanayokikabili chuo hicho, badala yake anataka kuona yanapatiwa ufumbuzi wa kudumu, hata kama ni kuikumbusha Wizara ya Elimu, zaidi ya mara tatu.

Makinda, aliteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan, wiki mbili zilizopita kuwa mkuu wa chuo hicho, baada ya Spika wa zamani na Katibu Mkuu wa CCM mstaafu, Pius Msekwa, kuhudumu katika nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka 10.

Akizungumza juzi chuoni hapo, wakati wa makabidhiano rasmi ya ofisi na vitendea kazi, Makinda, alisema baraza la chuo hicho linapofikiria kwamba kuna jambo la kumshauri, wasisite kufanya hivyo, kwa kuwa anachotaka yeye ni kupeleka gurudumu la maendeleo ya MoCu mbele zaidi.

"Baraza la Chuo mjiamini, pale mnapofikiria tunatakiwa kushauriana, Makamu Mwenyekiti na Mwenyekiti tuwasiliane. Tusilaze matatizo, tuwe tunayafahamu na kutafutia ufumbuzi.

"Hata kama kule wizarani mmesema, najua kuna Mwakilishi wa Wizara ya Elimu, kuna Mwakilishi wa Hazina (Wizara ya Fedha) hapa. Hata kama ukiwaambia mara tatu waambieni kuliko kusema atakuwa anajua.

...Mwambie hata kama ni Mjumbe wa Baraza na sisi wote mtuambie tuweze kusukuma gurudumu letu mbele zaidi ili chuo chetu kiwe cha mfano wa chuo cha kuigwa na mtu aseme natamani kwenda kusoma kule."

Aidha, Makinda, ameeleza kufurahishwa na uwekezaji mkubwa wa majengo na miundombinu ya MoCU, akisema baada ya kuteuliwa na Rais Samia, alidhani atakuta magofu kwa kuwa chuo hicho kilijengwa enzi za uhuru.

"Najifunza kwa haya mafanikio yenu kwamba ni watu ambao mmeamua kufanya kazi kwa uzalendo. Niliwaambia nilipozungumza jana na jumuiya ya wanachuo, kwamba mafanikio yeyote hayawezi kukosa changamoto," alisisitiza.

Katika hafla hiyo, Makinda, alikabidhiwa Sheria ya Vyuo Vikuu, Namba 7 ya Mwaka 2005, Haki Idhini ya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi na kuvishwa joho la mkuu wa chuo hicho kwa ajili ya kutunuku vyeti mbalimbali.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha MoCU, Prof. Alfred Sife, alisema utaratibu huo umeandaliwa kwa kuzingatia ukweli kuwa mamlaka ya uteuzi wa Mkuu wa Chuo na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo ni wa Rais Samia.

Alisema: "Kinachofanyika si kuwasimika viongozi hawa, maana hakuna mwenye mamlaka ya kufanya hivyo hapa, isipokuwa tunawakabidhi ofisi zao, mheshimiwa Rais alipoteua alisema kabisa uteuzi huu unaanza lini."



Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Seuta iliyopo Kata ya Songe, Wilaya ya Kilindi, Mkoa wa Tanga, Papias Kohoye, akipiga magoti katika umati wa watu waliohudhuria mahafali ya 26 shuleni hapo jana huku akiwa amekumbatia nyaraka zenye kero mkononi mwake, alimshukuru Rais Samia Hassan Suluhu kwa kuisaidia shule hiyo zaidi ya Sh. milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba tatu za walimu, ukarabati madarasa nane na matundu ya vyoo. **PICHA: DEGE MASOLI**

# DC awaagiza TARURA kujipanga na mvua za El-Nino

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Karatu, Dadi Kolimba, amewaagiza watumishi wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Mkoa wa Arusha, kutatua kero za ubovu wa miundombinu ya barabara, kabla ya mvua za El-Nino zinazotarajiwa kuanza wakati wowote.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati akifungua kikao kazi cha watumishi hao kinachofanyika kwa siku mbili wilayani humo.

Alisema taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa Nchini (TMA), kuhusu kuwapo kwa mvua hizo, zinatolewa kila wakati, huku akihimiza kila idara kujipanga kutatua matatizo yaliyopo kwenye maeneo yao kabla na baada ya mvua hizo kuanza.

Aidha, alisema kuna shughuli ambazo zinatakiwa kufanyika kabla ya maafa, lakini kunashughuli zinatakiwa kufanyika wakati wa maafa na kuna shughuli ambazo zinatakiwa kufanyika baada ya maafa na sekta hiyo ni muhimu katika kuepushia wananchi na maafa.

"Maeneo ambayo yamekuwa na matatizo mkayaweke vizuri kwa kuzibua mitaro, kuweka makaravati kabla ya athari kubwa haijatokea, tuweke mipango yetu sawa na tuisimamie ili mvua zinapokuja tusipate madhara makubwa," alisema.

Vilevile, alisema kila mtu ana jukumu la kuona barabara zote za vijijini na mijini zimekaa vizuri ili kusaidia kusitokee maafa makubwa katika maeneo yao hasa na pale maafa yatakapotokea.

Alisema hakuna sababu ya kushindwa kuboresha barabara kwa kuwa serikali imeongeza utoaji wa bajeti na alipoingia wilayani humo mwaka 2021, walipata Sh. milioni 928.

Lakini kwa mwaka wa fedha 2022/23 wameanza kupata Sh. bilioni 2.3, huku Wilaya ya Karatu, ikiwa na mtandao wa barabara wenye kilometa 712.

Alisema kwa ushirikiano huo wataenda mbali zaidi kuimarisha barabara zao, lakini barabara ambazo zimetengenezwa kwa kiwango cha changarawe nikaribia km 166, hivyo waliishukuru serikali kwa fedha nyingi zinazoletwa katika wilaya hiyo.

Kaimu Meneja wa TARURA, Mkoa wa Arusha, Albart Kyando, alisema wamepokea maelekezo ya Mkuu wa Wilaya na wameshaanza kuchukuwa tahadhari zote kwa kuandaa mpango mkakati kama taasisi wa kukabiliana na maafa.

# Walimu sasa kuandaa vipindi, kufundisha kidijitali

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

TAASISI ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, imezindua Kituo cha Elimu kwa njia ya kidijitali (C-CoDE) ambacho kimegharimu Dola ya Marekani 100,000, kitatumika kwa ajili ya walimu kuandaa vipindi vitakavyofundishwa kidijitali.

Hayo yamesemwa jana jijini Arusha na Makamu Mkuu wa Taasisi hiyo, Prof. Maulilio Kipanyula, wakati akizungumza katika uzinduzi huo.

Prof. Kipanyula alisema kituo hicho kitatumika kufundisha walimu na wakufunzi kutoka vyuo mbalimbali nchini kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kufundisha kidijitali.

Kadhalika, alisema kituo hicho kimefadhiliwa na Serikali ya Uswisi kwa kushirikiana na vyuo viwili kutoka Uswisi na Morocco na kitakuwa msingi na cha kihistoria.

"Elimu ya kidijitali inawezesha watu kupata maarifa kwa usawa wakiwa popote nchini na kituo hiki, kitakuwa ndio mwarobaini wa kuleta chachu kwa taasisi zingine nchini, kuanza kutoa elimu kidijitali na tulikuwa tunatamani kutoa elimu kidijitali kwa muda mrefu," alisema.


Mkurugenzi wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof.Ladslaus Mnyone, alisema kitendo kilichofanywa na taasisi hiyo kinapaswa kupongezwa na kuigwa na taasisi zingine nchini kwa sababu serikali kwa sasa inasisitiza taasisi na vyuo kuwekeza katika kutoa elimu kidijitali, ili kumfikia kila mmoja popote alipo.

Aidha, alisema nafasi ya teknolojia ni ya muhimu, katika taasisi mbalimbali kwani zinawezesha utoaji wa elimu kwa haraka na kumfikia mhusika kwa njia rahisi, akiwa sehemu yoyote na kuweza kupata vijana wenye umahiri wa hali ya juu.

"Kuna wadau wengi wanahitaji kuunga mkono juhudi za serikali, tunawakaribisha, milango ipo wazi kwa ajili ya kufanya majadiliano na kuangalia namna ya kufanya na kuhakikisha kila kijana wa kitanzania anapata elimu akiwa mahali popote pale," alisema .

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo -Utafiti (UDSM), Prof. Nelson Boniface, alisema kupitia kituo hicho Watanzania wengi watapata elimu kwa njia ya kidijitali kwani ni kituo cha mfano na ni cha kipekee nchini.

Alisema: "Kuna vituo vitatu tu kwa Afrika Mashariki na hiki ni kituo cha kwanza kwa Tanzania kinachotoa elimu kwa njia ya kidijitali, ili kuwafikia Watanzania wengi walioko katika maeneo mbalimbali ya mjini na vijijini, pia sisi tumekuja kujifunza kwa wenzetu ili tushirikiane nao."



## HABARI KANDA YA ZIWA




Meneja wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) Mkoa wa Kahama, Aisha Nyemba (kulia), akimkabidhi cheti cha pongezi Mwasibu wa Kampuni ya Taifa Mining and Civils Ltd, Evans Nyamwesa, kwa uchangiaji mzuri wa michango ya wanachama ya kila mwezi, jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# TBS yaombwa kufanya ukaguzi wa kushtukiza kubaini bidhaa feki

**Na Halima Ikunji,** KALIUA

KAIMU Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Kaliua Mkoa wa Tabora, Gibson Milambo, amelishauri Shirika la Viwango Nchini (TBS), kufanya ukaguzi wa kushtukiza mara kwa mara ili kubaini bidhaa zisizo na viwango.

Alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki wakati wa kampeni ya elimu kwa umma iliyoendeshwa na shirika hilo kwa zaidi ya wananchi 5,615 kutoka maeneo mbalimbali ya Halmashauri ya Wilaya za Igunga, Kaliua, Sikonge, Uyui na Manispaa ya Tabora.

Alisema TBS inafanya kazi nzuri ya kuwabaini watu wanaouza bidhaa zisizo na viwango, lakini ni muhimu wakawa na utamaduni wa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kuwalinda walaji dhidi ya bidhaa hafifu.

Kupitia kampeni hiyo ya elimu kwa umma, TBS ilihamasisha wajasiriamali wadogo kuthibitisha ubora wa bidhaa zao na wafanyabiashara kusajili maduka ya chakula na vipodozi.

Kadhalika, kampeni hiyo ya elimu kwa umma ilifanyika katika maeneo mbalimbali yakiwamo ya sokoni, stendi, minadani na maeneo mengine ya wazi, ambapo wananchi walijitokeza kupata elimu na ufahamu wa masuala mbalimbali yahusuyo ubora wa bidhaa.

Akizungumza wakati wa kampeni hiyo, Meneja Uhusiano na Masoko TBS, Gladness Kaseka, alisema lengo la TBS ni kutoa elimu kwa umma katika ngazi za wilaya zote na mpaka sasa wameshazifikia wilaya 72.

Naye Mkaguzi wa TBS, Magesa Mwizarubi, aliwasisitiza wajasiriamali na wafanyabiashara kuhakikisha wanauza bidhaa zilizothibitishwa ubora.

Magesa aliwafafanulia wananchi umuhimu wa viwango katika maisha yao ya kila siku na kuwataka wawe mabalozi wa kuhamasisha ubora ndani ya jamii wanakoishi sambamba na kutoa taarifa katika ofisi ya TBS zilizopo karibu.

Hivyo, aliwataka wajenge utamaduni wa kupiga simu katika kituo cha huduma kupitia mawasiliano yaliyotolewa iwapo watakutana na changamoto zinazohusu masuala ya ubora wa bidhaa wakati wa manunuzi.

# SGA yapewa tuzo ya ulinzi wa kisasa migodini

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

KAMPUNI ya ulinzi ya SGA imepokea tuzo kwa utoaji wa huduma bora za ulinzi unaotumia teknolojia ya kisasa migodini.

Tuzo hiyo ilitolewa wakati wa Maonesho ya Sita ya Kimataifa ya Madini yaliyomalizika mkoani Geita hivi karibuni, kufungwa na Makamu wa Rais wa Pili Zanzibar, Hemed Suleiman, washiriki zaidi ya 350 walihudhuria.

Katika maonyesho hayo, washiriki hao walipata fursa ya kushuhudia jinsi gani teknolojia na binadamu vinaweza kutumika kwa pamoja katika masuala ya ulinzi wa mali migodini.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kupokea tuzo hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa SGA, Eric Sambu, aliwapongeza waandaaji wa maonesho hayo kwa maandalizi mazuri na kwa kutambua mchango wa SGA.

"Tuzo hii inadhihirisha juhudi zetu katika kuhakikisha ulinzi na usalama wa kutosha katika maeneo ya migodi ili wahusika wakuu katika eneo hilo wajikite vikamilifu katika biashara," alisema.

Alisema kampuni hiyo imewekeza sana katika ubia na kampuni kubwa yanayotengeneza vifaa vya ulinzi wa kielektronia ili kuhakikisha wateja wa SGA wanapata huduma bora kwa bei nafuu.

"Siri yetu kuu ni mafunzo tunayotoa kwa mafundi wetu ili waendelee kuwapa wateja huduma bora inayoendana na fedha walizowekeza katika teknolojia hizi," alisema.

Alisema SGA ilitambuliwa na Wizara ya Madini mwaka jana pia katika warsha ya madini kwa kuthamini vitu vya ndani ya Tanzania.

Sambu alisema SGA ilikuwa kampuni ya kwanza kuanzisha utoaji wa huduma binafsi za ulinzi nchini miaka 40 iliyopita, kwa sasa imeajiri wafanyakazi wa kitanzania wapatao 5,000 katika matawi yake yote nchini.

# TRA yasisitiza utoaji risiti halali mauzo ya bidhaa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Shinyanga, wamewataka wafanyabiashara mkoani hapa kuhakikisha wanatoa risiti halali za mauzo ya bidhaa kwa wateja.

Pia imewakumbusha wananchi kudai risiti pindi wanaponunua bidhaa mbalimbali ikiwa ni sehemu ya wajibu wao ili kuepukana na kadhia mbalimbali wanazoweza kukumbana nazo ikiwa ni pamoja na faini.

Meneja wa TRA Mkoa wa Shinyanga, Faustine Mdessa, aliyasema hayo wakati kilele cha Wiki ya Huduma kwa Wateja na kusema kuwa utoaji wa risiti halali ni kuiwezesha serikali ipate mapato sahihi kupitia kodi na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

"TRA tunawasihi wafanyabiashara wasiibie serikali, bali watoe risiti halali za mauzo ya bidhaa kwa wateja, pia tunawasihi wananchi wanapokuwa wakinunua bidhaa wachukue risiti halali, tukimkamata mtu hajachukua risiti halali faini yake ni asilimia 20 ya mauzo ya bidhaa zake," alisema Mdessa.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Johari Samizi, alisema nchi yoyote ambayo imepiga hatua kubwa kimaendeleo wananchi wake ni walipaji wa kodi wazuri na kuwasihi wafanyabiashara wasikwepe kulipa mapato ya serikali, bali walipe kwa hiari yao kwa maendeleo ya Taifa.

Pia aliwataka wananchi kukataa tabia ya baadhi ya wafanyabiashara kuwapatia risiti za kusindikiza mzigo, ambazo hazina uhalisia wa kiwango halisi cha fedha ambazo wamenunua bidhaa zao, kwamba kitendo hicho ni kuiibia mapato serikali.

# NSSF yawaonya wanaoghushi barua ili kupata mafao

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) Mkoa wa Kahama, umetangaza kiama kwa waajiriwa wanaoghushi barua za kufukuzwa kazi na kuziwasilisha NSSF kwa lengo la kujipatia mafao wakati bado wako kazini.

Meneja wa NSSF, Asha Nyemba, alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na waajiri pamoja na wanachama wa mfuko huo, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya kilele cha wiki ya huduma kwa mteja yenye kauli mbio "Ushirikiano kwa huduma bora".Alisema kuna baadhi ya wajiriwa wasiokuwa wadilifu hususani vijana ambao wamekuwa na tabia ya kughushi barua za kuondolewa kazini na kuambatanisha katika maombi ya kutaka fedha zao NSSF.

Alisema wanapofuatilia uhalali wa barua hizo wanabaini hazijatoka kwa waajiri, kwamba bado wanaendelea na kazi.

Nyemba alisema kujaribu kupata mafao bila kuwa na sifa iliyoainishwa kwa mujibu wa sheria ni kosa, akisema watakaobainika watachukuliwa hatua.

"Tunapopokea maombi ya mwanachama wetu kuhitaji mafao yake na huku hana sifa na anauwezo wa kutafuta kazi nyingine na kuendelea na michango yake, huwa lazima tufuatilie kule alipotoka kujua ni kweli kile alichowasilisha au laa na ndio sababu ya kuwapatia muda," alisema Nyemba.

Kaimu Meneja wa Mfuko huo, Shabani Mbwana, alisema lengo la michango inayokatwa na kuwasilishwa na waajiri ni kuwasaidia waajiriwa pale wanapostaafu.

Alisema ili waweze kulipa mafao vema kwa mwanachama aliyestaafu ni lazima awe amesajiliwa na kuwa na namba ya uanachama na mwajiri wake amelipa michango sahihi kila mwezi na kwa wakati.

Akizungumza kwa niaba ya waajiri, Mwasibu wa Kampuni ya Taifa Mining and Civils Ltd, Evans Nyamwesa alisema, kila mwajiri amekuwa akihakikisha anawasilisha michango ya wafanyakazi wake kwa wakati na kuahidi kutoa ushirikiana wa kuwabaini wale wanaoghushi barua za kukosa ajira.

Nipashe
Spotika



NJIA 3 ZA CHELSEA KUMALIZA KABISA UKAME WA MABAO UK. 12-13




# WASHAMBULIAJI WATANO BORA WANAOSAIDIA TIMU

**LONDON,** England

JUKUMU la washambuliaji katika soka limebadilika kwa kiasi kikubwa baada ya muda na mabadiliko makubwa kuelekea kuenea kwa washambuliaji. Hapo awali, washambuliaji wa kati wa jadi kimsingi walikuwa ndio wafungaji wa mabao, ambao umakini wao ulikuwa katika kufunga tu.

Lakini mchezo wa kisasa unadai utofauti zaidi kutoka mbele. Washambuliaji wanaounga mkono, ambao mara nyingi hujulikana kama washambuliaji wa pili au washambuliaji wa 'uwongo', wameenea sana katika mchezo wa kisasa.

Wachezaji hawa si tu wanachangia mabao, lakini wanafanya vema katika uchezaji, kushuka zaidi ili kuunganisha mchezo, kutengeneza nafasi kwa wenzao na kuwezesha ushambuliaji wa jumla wa timu. Makala haya yanachambua washambuliaji watano bora wanaosaidia katika soka la kisasa duniani.

**#5. Marcus Thuram (Inter Milan)**

Marcus Thuram alikuwa mmoja wa wachezaji huru wa hadhi ya juu katika soko la uhamisho msimu wa majira ya joto. Amejitengenezea jina kutokana na uhodari wake na uwezo wa kucheza katika nafasi nyingi kwenye mstari wa mbele.

Sifa za kimwili za Thuram pamoja na ubora wake wa kiufundi, humwezesha kuwazidi nguvu wapinzani na kuwaleta wachezaji wenzake kucheza. Baada ya kuja kama winga, amebadilika na kuwa mshambuliaji wa kati hivi karibuni. Lakini Thuram si namba tisa ya kitamaduni.

Ni mwanasoka mwenye akili nyingi na ana uwezo wa kutengeneza nafasi za mabao kwa wachezaji wenzake. Thuram pia ana uwezo wa kufumania nyavu mara kwa mara na ni mmoja wa washambuliaji wanaosapoti, bora duniani hivi sasa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, amefunga mabao mawili na kutoa pasi nne za mabao katika mechi saba kwenye mashindano yote akiwa na 'Nerazzurri' hadi sasa msimu huu.

**#4. Joao Felix (Barcelona)**

Joao Felix ni mmoja wa washambuliaji wenye vipaji vya asili katika kizazi chake. Ustadi wake wa kiufundi ni wa kiwango cha juu. Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ureno ameonesha uwezo wa kipekee kama mshambuliaji msaidizi.

Maono na akili yake ya soka inamwezesha kuusoma mchezo kwa ufasaha, kupiga pasi za kuvutia na kutengeneza nafasi za mabao kwa wachezaji wenzake. Zaidi ya hayo, ustadi wake wa kucheza chenga na udhibiti wa karibu humruhusu kujinasua na kuwashinda wapinzani wake mara kwa mara.

Nguvu na ubunifu wake vinamfanya kuwa mtaji wa thamani kwa timu yoyote na anatarajiwa kuimarika akiwa Barcelona, ambapo kwa sasa yuko kwa mkopo kutoka Atletico Madrid. Amefunga mabao matatu na kutoa pasi mbili za mabao katika mechi tano alizocheza kwenye michuano yote akiwa na Barca hadi sasa msimu huu.

**#3. Cody Gakpo (Liverpool)**

Cody Gakpo anaonekana kuimarika katika Klabu ya Liverpool na anatajwa kuwa na mchango mkubwa kwa 'Wekundu' hao msimu huu. Fowadi huyo wa Uholanzi ni bora katika maana ya kiufundi na uhodari wake kama mshambuliaji unamfanya kuwa tegemeo la kusisimua la kucheza pamoja.

Gakpo mara nyingi 'huteleza' na kutengeneza fursa kwa wachezaji wenzake kutokana na ustadi wake wa kuendeleza mpira, uwezo wa kupiga pasi na kuona. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, amekuwa mchezaji wa kutegemewa wa kufunga mabao kwa Timu ya Taifa ya Uholanzi na anatarajiwa kupata mafanikio zaidi akiwa na Liverpool.

Amefunga mabao mawili katika mechi saba alizoichezea Liverpool hadi sasa msimu huu. Gakpo alifunga mabao saba na kutoa pasi tatu za mabao katika mechi 21 za Ligi Kuu England akiwa na Liverpool msimu uliopita baada ya kujiunga na klabu hiyo Januari 2023.

**#2. Julian Alvarez (Manchester City)**

Julian Alvarez alikuwa mmoja wa nyota waliochipukia msimu wa 2022-23. Aliichezea Argentina katika Kombe la Dunia la 2022, akifunga mabao manne na kuchukua jukumu muhimu katika mafanikio yao kwenye hatua kubwa zaidi ya yote.

Alvarez alifanya kazi nzuri kwa Manchester City pia, mara nyingi akichukua nafasi ya Erling Haaland. Lakini wasifu wa mshambuliaji huyo mchanga wa kati wa Argentina ni tofauti sana na ule wa Haaland.

Alvarez anahusika zaidi na ujenzi na anaweza kuchangia kwa njia mbalimbali pamoja na kufunga mabao kwa timu yake. Ametuhumiwa kama mshambuliaji msaidizi msimu huu katika Klabu ya Manchester City na anaonekana kuimarika katika nafasi hiyo.

Katika mechi 10 kwenye michuano yote kwa City hadi sasa msimu huu, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, amefunga mabao manne na kutoa pasi nne za mabao.

**#1. Lionel Messi (Inter Miami)**

Lionel Messi ndiye namba tisa ya uongo ya wakati wote. Ameurudisha jukumu hilo katika klabu yake mpya ya Inter Miami na amekuwa katika hali ya juu sana kwa timu hiyo ya Ligi Kuu ya Marekani tangu ajiunge nayo msimu huu wa majira ya joto.

Uwezo wa Messi wa kufunga mabao na uchezaji ni wa kiwango cha kimataifa na amebadilisha hali ya Inter Miami tangu ajiunge nayo. Mshindi huyo mara saba wa Ballon d'Or, amefunga mabao 11 na kutoa pasi tano za mabao katika mechi 12 katika mashindano yote akiwa na Inter Miami hadi sasa msimu huu.

## ISIKUPITE

MABAO mawili Jude Bellingham aliyoifungia Real Madrid juzi katika ushindi wa 4-0 kwenye LaLiga dhidi ya Osasuna, yanamfanya nyota huyo wa England kumpiku Cristiano Ronaldo kwa kuhusika kwenye mabao mengi (12) ndani ya mechi 10 za mwanzo tangu ajiunge na timu hiyo. Ronaldo alifunga mabao 10 na asisti moja, wakati Bellingham kwa mechi hizo amewafungia 'Los Blancos' hao mabao 10 na asisti mbili.



## Extra Time



# NJIA 3 ZA CHELSEA KUMALIZA KABISA UKAME WA MABAO



CHELSEA

**LONDON,** England

CHELSEA haiwezi kupata mapumziko kwa sasa. Mabao matano katika mechi sita za Ligi Kuu England kabla ya mwishoni mwa wiki kupata manne zaidi dhidi ya Burnley kwenye mechi yao ya nane ya msimu, si alama ya timu ambayo ilishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya miaka miwili tu iliyopita.

**Hata hivyo, hilo limekuwa kosa lao tangu kuondoka kwa kocha Thomas Tuchel kiasi kwamba wako karibu sana na kushuka daraja kuliko kuwa nafasi nne za juu.**

Mada inayojirudia wakati wa mbio hizi mbaya imekuwa kukosa uwezo wa kupata goli kwa urahisi. Msimu uliopita ulikumbwa na ukosefu wa kasi ya juu kwani walifunga mabao 38 pekee kwenye Ligi Kuu England.

Inafurahisha kabla ya ushindi wao wa mwishoni mwa wiki, Erling Haaland pekee ndiye alikuwa amefunga mabao mengi zaidi ya Ligi Kuu (44) kuliko Chelsea yote (43), tangu aanze kuichezea kwa mara ya kwanza Manchester City.

Kinachosikitisha zaidi ni kwamba hakuna mchezaji wao aliyevuka alama ya tarakimu mbili wakati wa msimu mzima. Kai Havertz alikuwa mchezaji wao aliyefunga mabao mengi zaidi msimu wa 2022-23 (mabao tisa) na aliondoka kwenda Arsenal msimu wa majira ya joto.

Licha ya kuwasili kwa Mauricio Pochettino, Chelsea wameendelea kutokuwa na uwezo mbele ya lango. 'The Blues' tayari wako nje ya kinyang'anyiro cha ubingwa msimu huu na wako nyuma kwa pointi tano kutoka nafasi nne za juu. Kwa wakati huu, hata kufuzu kwa Ligi ya Europa inaonekana kuwa ngumu.

Je, Chelsea wanaweza kufanya nini ili kumaliza matatizo yao ya kufunga mabao? Hebu tuangalie njia tatu ambazo zinaweza kuwafanya wamalize kabisa ukame wa mabao...

### #3. Kumtumia Armando Broja

Armando Broja alikuwa akipata muda wa kutosha wa kucheza mara kwa mara chini ya makocha Thomas Tuchel na Graham Potter kabla ya kupata jeraha Desemba mwaka jana na kusimamisha kasi yake. Hata hivyo, anaweza kutoa ushindani unaohitajika sana kwa Nicolas Jackson ambaye amekuwa na wakati usio wa kawaida katika kipindi chake kifupi kwenye klabu hiyo.

Masuala ya kinidhamu pia yanamtia wasiwasi Jackson, ambaye amepata kadi tano za njano katika mechi zake sita alizoichezea klabu hiyo.

Chelsea tayari wamekumbana na vikwazo vingi linapokuja suala la majeruhi msimu huu. Hawawezi kumudu kupoteza wachezaji kwa sababu ya kusimamishwa au masuala ya kinidhamu, hasa katika mstari wa mbele.

Kurejea kwa Broja kunaweza kuwa habari njema kwa Pochettino. Ingawa hajawahi kuwa hodari kama washambuliaji wakubwa wa Chelsea wa zamani, anaweza kutoa ushindani muhimu kwa Jackson pale mbele.

Uhamisho wake wa mkopo kwenda Southampton msimu wa 2021-22, ulikuwa wa matumaini kwa mchezaji mchanga. Alifunga mabao tisa kwa kikosi kilichomaliza katika nafasi ya 15 kwenye Ligi Kuu msimu huo.

Chelsea itahitaji mabao kutoka kwa wachezaji wote wa kikosi. Ikiwa Broja kwa namna fulani ataweza kunyakua kasi na kufunga takriban mabao 10-15 msimu huu, na anaweza kuirudisha meli ya Chelsea kwenye usawa wake pale Stamford Bridge.

### #2. Kiungo wa kati kutengeneza mashambulizi

Ingawa upangaji wa safu ya ulinzi na ukosefu wa ubunifu wa mbele umezuia mashambulizi ya Blues, safu yao ya kiungo haijasaidia hata kidogo katika kufanya mambo kuwa bora zaidi. Uteuzi duni wa wachezaji haujamsaidia Pochettino kwani amechagua kuwapanga Enzo Fernandez, Conor Gallagher na Moises Caicedo katika safu ya kati.

Wakati Fernandez ameanza msimu akiwa katika hali nzuri, anafaa zaidi kwa nafasi ya kiungo wa kati. Anaweza kuwekwa pamoja na kiungo mkabaji Caicedo na nyuma ya mfungaji mabao namba 10.

Conor Gallagher ametatizika katika safu ya kiungo msimu huu na itakuwa bora ikiwa Pochettino atamweka benchi kwa sasa. Ingawa The Blues watakosa sana kiwango chake cha kazi, wanahitaji ubora fulani kwenye mpira ili kufungua safu ya ulinzi.

Ikizingatiwa kutojiamini kukithiri kwa safu yao, jukumu litakuwa kwa viungo na safu ya mbele kufanya kitu kifanyike katika nafasi ya tatu ya mwisho. Na kwa kuwa wanakosa mshambuliaji wa kati wa kutegemewa, Chelsea watahitaji kutengeneza nafasi nyingi zaidi kutoka safu ya kiungo ili kuwazidi wapinzani wao.

### #1. Kutumia mfumo wa 4-2-3-1

Wakati akiwa Tottenham Hotspur, Pochettino alijenga sifa yake kwa kutumia mfumo wa 4-2-3-1. Lakini tangu alipowasili Chelsea, amekuwa akipendelea mfumo wa ulinzi zaidi wa 3-4-2-1. Pochettino anajulikana kwa aina yake ya soka ya kasi na ya kushambulia.

Kwa kuwa Chelsea walicheza sana mfumo wa 3-4-2-1 chini ya Thomas Tuchel na Graham Potter, Pochettino anaweza kujaribu kuutumia mfumo huo kuifanya timu iendelee na kukimbia.

Kando na hilo, jeraha la Christopher Nkunku limefanya mambo kuwa mabaya zaidi kwao. Mfaransa huyo angekuwa bora kwao kama namba 10 katika mfumo wa 4-2-3-1. Misimu yake miwili iliyopita pale RB Leipzig alitoa mchango wa mabao zaidi ya 85, na wanakosa sana ubunifu na uamuzi wa mapema.

Hata hivyo, sio kana kwamba wana London wana uhaba wa chaguzi mapema. Mara kwa mara, Pochettino amemtumia Enzo Fernandez katika nafasi za juu kuimarisha mashambulizi yake. Lakini akiwa na Cole Palmer, tayari ana chaguo ambalo linaweza kumwachia Muargentina huyo, ambaye kuna wakati anacheza kama namba tisa.

Muingereza huyo ameonekana mkali wakati akitokea benchi kwa The Blues. Kusogea kwake kati ya mistari kwa haraka kunaweza kuwapa Chelsea nafasi nzuri zaidi ya kufunga mabao.

## Nukuu

"Ushindi mzuri hekaluni! Takwimu mbili," **Mshambuliaji wa Manchester City, Erling Haaland, akimpongeza mchezaji mwenza wa zamani wakiitumikia Borussia Dortmund, Jude Bellingham, baada ya kuipiku rekodi ya Cristiano Ronaldo ndani ya Real Madrid ya mabao 10 na asisti moja kwenye mechi 10 za mwanzo tangu ajiunge nayo, wakati Muingereza huyo juzi alifikisha mabao 10 na asisti mbili kwa idadi hiyo ya mechi.**



"Ni kazi yake, hapana? Kucheza vizuri. Wachezaji wote wanajaribu kucheza vizuri na leo [juzi] alikuwa vizuri. Alihusika katika mabao na nina furaha kwake na nina furaha kwa timu. Timu ilikuwa nzuri, kiwango kizuri, wanastahili sifa. Furaha kwao na kwenda mapumziko ya kimataifa na hisia tofauti hadi mwisho," **Kocha wa Chelsea, Mauricio Pochettino, akimsifu winga Raheem Sterling kwa kuonesha kiwango kizuri pamoja na timu kwa ujumla baada ya ushindi wa mabao 4-1 ugenini dhidi ya Burnley juzi, Jumamosi.**



"Kwenye mpira ni kuliwa au kula. Mara nyingi sana katika kipindi cha kwanza cha msimu huu tuliliwa na wapinzani ambao wana njaa zaidi. Hii haiwezi kuendelea kuwa hivi, lazima iondoke. Kila mchezaji anapaswa kujitoa katika kila dakika anapokuwa uwanjani," **Kocha wa Manchester United, Erik ten Hag, akiwajia juu wachezaji wake wa baada ya ushindi wa dakika za lala salama wa mabao 2-1 dhidi ya Brentford juzi, Jumamosi.**





Mabingwa watetezi wa Ligi ya Mabingwa Afrika, Al Ahly

# USIYOYAJUA WAPINZANI SIMBA, YANGA LIGI MABINGWA AFRIKA

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara ya kwanza kwenye historia ya soka la Tanzania, timu za Simba na Yanga zinakwenda kucheza mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi kwa pamoja.

**Ni tofauti na miaka ya nyuma ambapo kila timu ilikuwa inacheza kwa msimu wake, lakini safari hii Tanzania ni moja kati ya nchi tatu zilizoingiza timu mbili kwenye hatua hiyo. Zingine ni Tunisia ambazo ni Etoile du Sahel na Esperance, na Misri iliyoingiza timu za Al Ahly na Pyramids.**

Ijumaa iliyopita nchini Afrika Kusini ilipangwa droo ya makundi manne ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba ikiwa Kundi B na Yanga kuangulia Kundi D.

Kwenye makala haya tutaziangalia na kuzichambua timu ambazo wawakilishi hao wa Tanzania wamepangiwa nazo, twende sasa...

### Al Ahly - Misri

Ipo Kundi D pamoja na Yanga. Mara ya mwisho Yanga kukutana nayo ni mwaka 2016, Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya raundi ya pili. Katika mechi hizo za mtoano, zilitoka sare bao 1-1 nchini na Yanga kufungwa mabao 2-1 ugenini, ikaangukia Kombe la Shirikisho alikofika hatua ya makundi.

Al Ahly ndiyo mabingwa wa kombe hili kwa sasa, na ni timu inayoogopesha zaidi kwenye michuano hiyo kutokana na historia yake.

Ina mataji 120 mpaka sasa, ikitwaa Ligi ya Mabingwa Afrika mara 13, Kombe la Shirikisho Afrika mara nne, Ligi Kuu nchini Misri mara 43, pamoja na makombe mengine kama FA, Super Cup ya Misri, Kombe la Mataifa ya nchi za Kiarabu, Kombe la Mfalme Hussein na mengine mengi, ambapo ikiyajumlisha unapata idadi hiyo.

Imeingia makundi kwa kutoa kichapo cha mabao 7-0 dhidi ya St George ya Ethiopia, ikishinda ugenini mabao 3-0, na nyumbani 4-0.

Mpaka sasa imecheza mechi moja tu ya ligi nchini kwao iliyo raundi ya tatu, ikiichapa Al Masry mabao 4-0, jana ikitarajia kucheza mechi ya pili dhidi ya Ismailia.

### Wydad Casablanca - Morocco

Kipindi kisichopungua miezi sita, Simba ilicheza mechi ya robo fainali Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Wydad Athletic Club ya Casablanca Morocco. Wydad imepangiwa tena kundi moja na Simba msimu huu hatua hiyo wakiwa Kundi B.

Mwishoni mwa Aprili mwaka huu, Simba ilishinda bao 1-0 nchini na kwenda kufungwa idadi kama hiyo ya na kutolewa kwa mikwaju ya penalti 4-3. Wydad ni wanafainali wa kombe hili ikifungwa mabao 2-1 ugenini dhidi ya Al Ahly, na kulazimishwa sare ya bao 1-1 nyumbani, wakiwaacha Wamisri wakiondoka na kombe.

Imefanikiwa kutinga hatua ya makundi kwa kuitoa Hafia ya Guinea kwa jumla ya mabao 4-1, ikilazimisha sare ya bao 1-1 ugenini, kabla ya kushinda mabao 3-0 nyumbani.

Inaongoza Ligi ya Morocco mpaka sasa ikicheza mechi sita, ikishinda nne, sare moja na kupoteza moja, ikijikusanyia jumla ya pointi 13.

### CR Belouizdad - Algeria

Ni mabingwa wa Algeria msimu uliopita na imefika hatua hiyo kwa kuibanjua Bo Rangers ya Sierra Leone jumla ya mabao 6-2, ikishinda mabao 3-1 nyumbani na ugenini. Imepangwa Kundi D na Yanga, ambapo ndiyo timu pekee kwa wawakilishi hao wa Tanzania ambayo haijawahi kukutana nayo. Imecheza mechi mbili tu kwenye Ligi Kuu mpaka sasa, ikishinda moja na kupoteza moja.

### ASEC Mimosas - Ivory Coast

Imepangwa Kundi B na itakwenda tena kukutana na Simba, lakini safari hii ni katika makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika na siyo Shirikisho.

Mwaka jana zilikuwa kwenye kundi moja la Kombe la Shirikisho, kila timu ikishinda nyumbani kwake, Simba ikishinda 3-1 nyumbani, nayo mabao 3-0 ugenini.

Imetumbukia kwenye makundi ikianza tangu hatua ya awali kwa kutoka suluhu ugenini dhidi ya Coton Sport ya Benin na kisha ushindi wa mabao 2-0 nyumbani na raundi ya kwanza iliifunga Al Ahly Benghazi ya Libya mabao 2-1 nyumbani, baada ya suluhu ugenini. Ligi ya nchini humo ilitarajiwa kuanza jana.

### Medeama - Ghana

Medeama ilishawahi kuwa kundi moja na Yanga Kombe la Shirikisho mwaka 2016. Safari hii wanakutana kwenye Kundi D Ligi ya Mabingwa Afrika. Mechi ya kwanza nyumbani, Yanga ililazimishwa sare ya bao 1-1, na ya marudiano, Medeama ilishinda mabao 3-1.

Medeama ilianzia hatua ya awali, ikiiondoa Remo Stars ya Nigeria kwa penalti 3-2, baada ya kila timu kushinda nyumbani bao 1-0, ikatinga raundi ya kwanza na kuiondosha Horoya ya Guinea kwa jumla ya mabao 4-3, ikishinda mabao 3-1 nyumbani na kufungwa ugenini 2-1. Imecheza mechi tatu za ligi ikishinda moja, sare moja na kupoteza moja, ikikusanya pointi nne.

### Jwaneng Galaxy - Botswana

Ni timu ambayo Watanzania wengi wanaikumbuka kutokana na kisa cha kuiondoa Simba kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika mwaka 2021.

Ndiyo timu iliyoitoa Simba kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, 2021 kwa kuichapa mabao 3-1, Uwanja wa Benjamin Mkapa na kuifanya kuangukia Kombe la Shirikisho ilikowenda kukutana na Asec Mimosas.

Katika mechi ya kwanza ugenini, Simba iliifunga Jwaneng Galaxy mabao 2-0, lakini ikajikuta ikipachikwa mabao 3-1 nyumbani, ikatoka kwa bao la ugenini matokeo ya jumla yakiwa 3-3. Sasa zote zimejikuta zipo kwenye kundi moja Ligi ya Mabingwa Afrika.

Ilitinga makundi kibabe dhidi ya Orlando Pirates ya Afrika Kusini kwa mikwaju ya penalti 5-4 baada ya kila timu kushinda bao 1-0 nyumbani. Ligi ya Botwana imeanza, lakini Jwaneng Galaxy haijaanza kucheza mechi yoyote mpaka sasa.

**JE, WAJUA?**



KABLA ya mechi ya jana, Manchester City ndiyo timu pekee ambayo Mikel Arteta, ameshindwa kuifunga kwenye Ligi Kuu England tangu aanze kuinoa Arsenal, amepokea vipigo katika mechi zote saba alizokutana na klabu yake hiyo ya zamani.



# Watumishi wa umma wapewa mbinu kuepuka mikopo umiza

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

WATUMISHI wa umma wametakiwa kujiunga na vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS) kwenye maeneo yao ya kazi, ili kuepuka kuingia kwenye mikopo umiza na nyonya damu.

Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Violet Mlinga, alisema hayo alipokuwa akifungua mkutano wa tatu wa MNRT SACCOS uliofanyika jijini hapa mwisho wa wiki.

Mlinga alisema watumishi wa umma wamekuwa wakirudishwa nyuma kimaendeleo kutokana na mikopo ya mitaani na watu binafsi au taasisi.

"Mimi binafsi ni mwanachama wa saccos hii na nimekuwa nikikopa na kurudisha mikopo yangu kwa wakati na nitaendelea kukopa kwa sababu ni riba ndogo na natoa wito kwa wengine kujiunga na huku," alisema.

Alibainisha kuwa mikopo umiza imesababisha baadhi ya wafanyakazi wengine kuwa na hali ngumu ya maisha kutokana na madeni pamoja na riba kubwa zinazotozwa huko.

Hivyo, aliwataka wanachama wa SACCOS hiyo kuwa waaminifu katika kurejesha mikopo waliyokopa ili mfuko usaidie wanachama wengine kupata mikopo hiyo.

Awali, Mwenyekiti wa NMRT SACCOS, Wilfred Msemo, alisema wanamtaji wa zaidi ya Sh.bilioni 1.9 na idadi ya wanachama iliyopo ni 390 kutoka maeneo mbalimbali hapa nchini.

Msema alisema SACCOS yao haibagui wanachama na inawakaribisha wafanyakazi wa wizara mbalimbali na taasisi zote nchini ili kujiunga.

Alieleza kuwa kuna baadhi ya wanachama wao wamefanikiwa kujenga nyumba, kununua magari, mashamba na wengine kuwekeza kwenye miradi mbalimbali ya kibiashara na ujasiriamali.

Msimamizi wa vyama vya ushirika Jiji la Dodoma, Yusuph Timotoli, alisema wamekuwa wakisimamia ipasavyo SACCOS na kuwachukulia hatua viongozi wasio waadilifu.

Alisema: "Uimara wa SACCOS unatokana na viongozi waadilifu waliopewa dhamana ya kusimamia rasilimali za chama na mali zilizopo, ikitokea viongozi wakakosa uadilifu tumekuwa wakiwaondoa kwenye nafasi zao na ikiwa amefanya ubadhilifu tunampeleka kwenye vyombo vya kisheria".

# RC aagiza wawekezaji wazawa kuongeza kazi ya uwekezaji

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amewataka wawekezaji wazawa kuongeza kasi ya uwekezaji katika maeneo mbalimbali jijini Dodoma ili kupanua wigo wa ajira kwa vijana na kuchangia pato la taifa.

Aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye uzinduzi wa tawi la kampuni ya wawekezaji wazawa ya Dar Ceramica.

"Tunaomba wawekezaji mjitokeze kwa wingi kuwekeza Dodoma lengo letu ni kuifanya Dodoma ya sasa kuwa tofauti na Dodoma ya zamani, lakini kupanua wigo wa ajira kwa vijana," alisema Senyamule.

Alisema ni muhimu wawekezaji wazawa kuchangamkia fursa zilizopo Dodoma kwa kuwa ina maeneo ya kutosha ya uwekezaji.

Naye Mkuu wa Masoko wa kampuni hiyo, Raymond Nkya, alisema kampuni hiyo mbali na kuuza vifaa vya ujenzi wamekuwa wakitoa ushauri wa kitaalamu wa matumizi sahihi ya vifaa ili kuepuka kutumia gharama kubwa.

Alisema kampuni hiyo imechangia mapato kwa mwaka Sh. bilioni 11 na kuahidi kuendelea kuunga mkono jitihada za serikali katika uwekezaji.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (katikati) na Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Alhaj Jabiri Shekimweri (kushoto), wakisikiliza maelezo kutoka kwa Mkuu wa Mauzo na Masoko wa Dar Ceramica Centre, Raymond Nkya, katika ufunguzi wa tawi jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wataka jamii ishirikishwe utungaji sera, sheria rasilimali asili

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WADAU wa mazingira nchini wameitaka serikali kuishirikisha jamii kwenye utungaji wa sera na sheria ili kurahisisha uhifadhi endelevu wa rasilimali asili.

Wameyasema hayo walipokutana kujadili matokeo ya miradi iliyofadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo (UNDP), chini ya Mfuko wa Mazingira Duniani (GEF).

Miradi hiyo 24, ni ile ambayo ni kipaumbele kwa jamii ambayo inahusu masuala ya ardhi, uendelezaji wa maeneo ya malisho, uhifadhi wa misitu na vyanzo vya maji, utunzaji wa mazingira.

Mratibu wa Programu ya Ruzuku Ndogo za GEF, Faustine Ninga, alisema katika kipindi cha miaka miwili tangu mwaka 2021, wamekuwa na miradi 24 ambayo imetekelezwa kwenye maeneo mbalimbali nchini na kukamilika Juni mwaka huu.

"Leo hii tumekutana ili kushirikishana matokeo ambayo tumeyaona kwenye miradi hii, changamoto na mambo ambayo tunaweza kujifunza kupitia utekelezaji wa miradi hii sasa na ujumbe gani wa kisera uliopatikana kupitia miradi hii," alisema.

Alisema miradi hiyo iliyokuwa na thamani ya Sh. bilioni 1.5, ilifadhiliwa na Mfuko wa Mazingira Duniani (GEF), uliopo chini ya Shirika la Kimataifa la Maendeleo (UNDP).

Alisema wanufaika wa miradi hiyo, wanatoka katika jamii kutoka mikoa ya Arusha, Simiyu, Morogoro, Mara, Manyara na Ruvuma.

Ninga alitaja vikwazo walivyoona wakati wa utekelezaji wa mradi huo ni uhitaji mkubwa wa ruzuku katika kutekeleza miradi ya jamii kwasababu mbalimbali ikiwamo mabadiliko ya tabia nchi, ujangili uhifadhi wa mazingira.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Jumuiko la Maliasili Tanzania (TNRR), Zackaria Faustine, alisema lengo la kukutana ni kushirikishana matokeo yaliyotokana na namna gani ya kutumia maarifa ya asili, kusimamia vyanzo vya maji, malisho misitu na wanyamapori na maeneo yenye ikolojia ya Tanzania.

"Tumejaribu kushirikisha serikali kuja kuona ni namna gani ya kutumia njia mbalimbali za kutumia, kutunza na kuendeleza maliasili za asili ili wakati wa maboresho ya sera na sheria waweze kutambua namna gani ya kumshirikisha mwananchi kusimamia rasilimali zake," alisema.

Faustine alishauri jamii ziendelee na njia zao za kukuza rasilimali za asili kwa ajili ya kizazi kilichopo na kijacho.

Mwakilishi wa Shirika lisilo la Kiserikali la Wanawake, (MIMUTE), Rose Njilo, aliwataka watunga sera kuhakikisha kuwa wanawashirikisha wananchi ili waweze kujumuisha mawazo ya wanaotumia sera.

Alisema: "Tumekuja kwa pamoja jamii za pembezoni ambazo ni jamii za kifugaji, wakulima na waokota matunda. Miradi hii imemgusa mwanamke moja kwa moja kwa kuwa ni miradi inayoshughulika na maji na malisho."





# Wananchi watoboa mabomba ya maji, wanyweshea mifugo

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

BAADHI ya wafugaji wilayani Mbarali katika Mkoa wa Mbeya, wanadaiwa kuhujumu miundombinu ya maji kwa kutoboa mabomba ili kunywesha mifugo yao,

Mwishoni mwa wiki Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alifanya ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali katika Wilaya ya Mbarali na kubaini hali hiyo, kwamba baadhi ya wafugaji hao wameanza kuhujumu mradi wa Ruduga- Mawindi.

Akizungumza na wananchi wa eneo hilo, Homera aliwatahadharisha kuacha tabia hiyo huku akiwaagiza viongozi kuwakamata wote wanaofanya vitendo hivyo na kuwachukulia hatua kali za kisheria ili kuwa fundisho kwa wengine wanaofanya hivyo.

Alisema mradi kwa mfugaji ambaye anataka kunywesha mifugo maji ya bomba anatakiwa kuvuta maji nyumbani kwake na kutengeneza bwawa ambalo ndilo atakuwa analitumia kunywesha mifugo badala ya kufanya uhuni wa kutoboa mabomba.

Alisema serikali imetumia fedha nyingi kutekeleza mradi huo kwa lengo la kuwakomboa wananchi wa vijiji vya Kata ya Mawindi ambao walikuwa wanahangaika kupata huduma hiyo na hivyo haiwezi kuwavumilia wanaohujumu.

"Mkiwakamata wachukulieni hatua kali bila kuwaogopa, mfugaji anaweza akauza ng'ombe mmoja akavuta maji nyumbani kwake ili aendelee kunywesha mifugo yake vinginevyo hatutawezi kuwavumilia wanaotoboa mabomba," alisema Homera.

Aidha, aliagiza Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Mbarali kupunguza gharama za kuwaunganishia wananchi kutoka Sh. 50,000 mpaka 25,000 ili wananchi wengi zaidi waunganishiwe huduma hiyo.

Akitoa taarifa ya uendeshaji wa mradi huo mwakilishi wa RUWASA, Brown Ngwazi, alisema umejengwa kwa gharama ya Sh. bilioni tano na unawanufaisha wananchi wa vijiji vitano ambavyo ni Itipigi, Manienga, Matemela, Mkadami na Ipwani ambavyo vyote vipo Kata ya Mawindi.

Alisema kimeundwa chombo maalumu cha uendeshaji ambacho kinaitwa Ruduga-Mawindi ambacho ndicho kinaendesha mradi huo na kwamba kina wajumbe wanne kutoka katika kila kijiji ambacho kipo kwenye mradi.

Alisema wananchi wanaotaka kuunganishiwa huduma hiyo, wanapatiwa vifaa kwa gharama maalumu na ambao wanataka kwenda kununua madukani pia wanaruhusiwa kununua.

"Gharama za awali kwa mwananchi ambaye anataka kuunganishiwa ni Sh. 206,500, hizi ni gharama za ufundi, fomu pamoja na vifaa lakini Sh.50,000 wanayolipa ni kwa ajili ya kujisajili," alisema Gwazi.

Mbunge wa Mteule wa Mbarali, Bahati Ndingo, aliomba mradi huo uwasaidie na wananchi wa Kata ya Igava ambao hawana maji na kwamba mradi huo wa Ruduga -Mawindi una maji mengi ambayo yanaweza kutosheleza na wananchi wa kata hiyo.

Alisema Wilaya ya Mbarali ina tatizo kubwa la maji na hivyo akaiomba serikali kuendelea kubuni vyanzo vipya vya maji ili kutatua kero hiyo ambayo ni ya muda mrefu.

Baadhi ya wananchi wa Kata ya Mawindi walisema kabla ya mradi huo, walikuwa wanatumia maji ambayo hawana uhakika na usalama wake kutokana na kuchangia na mifugo.

Mmoja wa wananchi hao, Bona Hussein, alisema wanawake walikuwa wanalazimika kuamka usiku kwenda kutafuta huduma hiyo kwenye makorongo hali ambayo ilikuwa inahatarisha maisha yao.

# Bashungwa: Barabara Iringa-Kilolo itachochea kilimo, utalii, biashara

**Na Elizabeth John,** IRINGA

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, amesema ujenzi wa Barabara ya Iringa-Kilolo (km 33.61) kwa kiwango cha lami wenye thamani ya Sh. bilioni 60.1 utakapokamilika utaleta mageuzi chanya ikiwamo kuchochea ukuaji wa sekta za kilimo, utali, biashara na uwekezaji.

Aliyasema hayo wiilayani Kilolo mkoani Iringa baada ya kushuhudia utiaji saini mkataba wa ujenzi wa barabara hiyo kati ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), na Meneja Mkazi kutoka Kampuni ya Hunan Construction Engineering Group.

"Hakika historia inaenda kuandikwa kwani Barabara ya Iringa - Kilolo imekuwa ni kilio cha muda mrefu, kutoka kwa waheshimiwa wabunge wa Mkoa wa Iringa na hasa wale ambao walikuwa wawakilishi wenu kupitia jimbo hili kwa nyakati tofauti tofauti pamoja na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi wameisemea sana barabara hii," alisema Bashungwa.

Alisema kuwa kujengwa kwa barabara hiyo kwa kiwango cha lami kutawezesha wananchi kiuchumi na kuwaondolea adha ya muda mrefu ya usafiri.

Hata hivyo, Bashungwa alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, anaifahamu adha ya wakazi wa Iringa na mikoa jirani katika eneo la Kitonga na amemwagiza kufika na timu ya wataalamu kutoka TANROADS na kufanya tathmini ya ujenzi wa barabara ya mbadala ya muda mfupi wakati serikali ikiendelea kutafuta dawa ya kudumu katika eneo hilo lenye mlima mkali.

Pia alisema Rais Samia ametoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya mchepuo ya Iringa (Iringa Bypass) yenye urefu wa kilometa 7.3 ambapo hivi sasa ipo katika hatua za manunuzi.

Bashungwa pia alizitaja barabara nyingine ambazo zitakwenda kujengwa kwa kiwango cha lami katika mkoa huo ikiwamo Barabara ya Iringa - Ipagala (km 71).

Wakati huo huo, Bashungwa aliwaagiza TANROADS kuusimamia kikamilifu ujenzi wa barabara hiyo ili ijengwe kwa viwango vilivyoainishwa kwenye mkataba ili kuweza kupata thamani halisi ya fedha ambazo serikali imewekeza ili barabara hiyo iweze kudumu kwa muda uliokusudiwa.

Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Injinia Mohamed Besta, alisema kuwa mradi huu utatekelezwa kwa muda wa miezi 24 kwa Sh. bilioni 60.1.

Alisema upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ulianza Februari 2019 na kukamilika Julai, 2021 na kufanywa na Kampuni ya Inter-Consult ya Tanzania na umezingatia vigezo vyote vya kitaalamu.

Alisema mradi huu ni moja ya miradi ambayo inatekelezwa na serikali ikishirikiana na Benki ya Dunia (WB) katika mradi wa Ushirikishaji na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi (RISE) ikiwa ni mikakati ya serikali ya kuhakikisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika mkoa wa Iringa.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akimtwisha ndoo ya maji mmoja wa wakazi wa Kata ya Mawindi wilayani Mbarali mwishoni mwa wiki alipokwenda kukagua mradi wa Ruduga-Mawindiambao uliojengwa kwa zaidi ya Sh. bilioni 5. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wazazi watajwa chanzo watoto vijijini kutopenda shule

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MJUMBE wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi Taifa anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela, amesema watoto wengi wa maeneo ya pembezoni mwa miji wanashindwa kuendelea na masomo ya sekondari baada ya kuhitimu elimu ya msingi kutokana na wazazi kutokuwa na mwamko wa elimu.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizindua kituo cha maandalizi ya masomo ya sekondari kwa wanafunzi waliohitimu darasa la saba mwaka huu katika Kata ya Iziwa jijini Mbeya, ambacho kitawanufaisha watoto wa kata hiyo ya Iziwa na Nsoho.

Alisema kutokana na hali hiyo aliamua kuanzisha vituo vya kuwaandaa wanafunzi wanaohitimu darasa la saba katika wilaya tatu ambazo ni Mbeya, Chunya na Rungwe ambazo ndizo zenye tatizo zaidi na kwamba kwa baadaye vituo hivyo vitakuwa katika wilaya zote za mkoa huo. Mwaselela alisema ataajiri walimu 20 ambao ndio watafanya kazi ya kuwaandaa wanafunzi hao kwa miezi mitatu kuanzia Oktoba mpaka Desemba ili Januari watakapokuwa wanaanza kidato cha kwanza wawe na mwanga.

Alisema walimu watakaoajiriwa ni wale ambao wamesomea fani hiyo lakini bado hawajaajiriwa ili na wao wanufaike kwa ajira hiyo ya muda mfupi.

"Nitawalipa mwenyewe mishahara kwa kutumia mapato ninayoyapata kwenye shule zangu za Paradise Mission na Patrick Mission, usaili wa walimu tutakaowaajiri utafanyika hivi karibuni ili waanze kazi," alisema Mwaselela.

Alisema serikali inagharimia elimu kwa watoto wote kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha sita na hivyo ni lazima kila mzazi aamke na kupeleka watoto shule.

Diwani wa Kata ya Iziwa, Kefas Sote, alimpongeza Mwaselela kwa uamuzi huo kwa maelezo kuwa watoto wengi wa maeneo hayo huwa wakihitimu darasa la saba hawapati maandalizi ya kujiunga na kidato cha kwanza kutokana na mazingira kuwa magumu.

Alisema wazazi wengi hawana uwezo wa kuwalipia watoto wao masomo hayo na hivyo kitendo cha kuwasaidia bure kitawasaidia kuanza kutumia kipato wanachopata kufanya maandalizi ya kujiunga kidato cha kwanza.

Alisema katika kata yake kuna watoto zaidi ya 100 ambao ndiyo wamehitimu darasa la saba na hivyo akawataka wazazi kuwapeleka watoto hao kwenye kituo ili wasome.



## Uongozi AAKIA watakiwa kuhakiki mashine za ukaguzi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

UONGOZI wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (AAKIA) umetakiwa kuhakikisha mashine zote za ukaguzi wa mizigo zinafanya kazi muda wote ili kuwarahisishia abiria wanao safari kupitia kiwanja hicho.

Waziri wa Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Khalid Salum Mohamed, alisema hatua hiyo itawarahisishia wasafiri wanaotumia kiwanja hicho kusafiri kwa urahisi bila ya usumbufu wowote.

Waziri huyo aliyasema hayo wakati alipofanya ziara maalum ya kukitembelea kiwanja hicho iliyolenga ukaguzi wa shughuli za operesheni zinazoendelea na pia kuangalia eneo ambalo linatarajiwa kujengwa jengo la jipya la abiria.

Akiwa eneo hilo, Dk. Khalid aliutaka uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuboresha mifumo ya kupozea joto katika kumbi hizo.

Pia aliitaka mamlaka hiyo na kushirikiana na Idara ya Uhamiaji kuongeza vizimba (sehemu za ukaguzi) vya uhamiaji kwa kuweka samani na mizigo kwa lengo la kurahisishia abiria kupata huduma za uhamiaji kwa haraka.

Wakati huo huo, Waziri huyo alitembelea barabara zinazoendelea kujengwa vijijini pamoja na kufika Kiboje Ghana kwa ajili ya kukagua hali ya barabara inayotarajiwa kujengwa hivi karibuni.

# Bei ya petroli, dizeli yazidi kupaa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BEI ya mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya ndege imezidi kupaa visiwani hapa kwa Oktoba ikilinganishwa na mwezi uliopita.

Akitangaza bei ya mafuta ambayo itaanza kutumika leo Oktoba 9, Meneja Uhusiano kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Mbarouk Hassan, alisema bei ya petroli kwa lita moja itauzwa kwa shilingi 3, 001 kutoka 2,950 bei ya awali.

Alisema kwa mafuta ya dizeli yatauzwa kwa shilingi 3,282 kutoka shilingi 3,012 ya mwezi uliopita.

Hassan alisema mafuta ya ndege nayo pia yamepanda kutoka shilingi 2,448 hadi shilingi 2,768, huku bei ya mafuta ya taa haijapanda ambayo yatauzwa kwa shilingi 2,921 bei ya awali.

Aidha, alisema sababu za kuongezeka kwa bei za mafuta ni kuongezeka kwa gharama za mafuta katika soko la dunia, gharama za uingizaji wa mafuta, uamuzi wa wazalishaji wakubwa wa mafuta duniani.

Alisema sababu zingine ni kupunguza uzalishaji na vikwazo vya kiuchumi ambavyo nchi ya Urusi imewekewa na mataifa ya magharibi.

Meneja huyo aliwataka wananchi kununua mafuta katika vituo halali vya mafuta na kudai risiti za kielektroniki kila wanaponunua mafuta.

Aidha, Meneja huyo alitaja vigezo vinavyotumika na mamlaka katika kupanga bei, ambavyo ni wastani wa mwenendo wa mabadiliko ya bei za mafuta duniani, gharama za uingizaji mafuta katika Bandari ya Dar-es-Salaam na Tanga.

Vingine ni thamani ya Shilingi ya Tanzania kwa Dola ya Marekani, gharama za usafiri, bima na 'Premium' hadi Zanzibar, kodi na tozo za serikali na kiwango cha faida kwa wauzaji wa jumla na reja reja.

Wakizungumza kuhusu kupanda kwa bei ya mafuta, watumiaji wa vyombo vya usafiri ikiwamo vya umma na biashara, walisema kupanda kwa bei hiyo kuna hatari ya kupanda bei kwa bidhaa zingine muhimu.

Haji Makame dereva wa bodaboda, alisema bei hiyo inakwenda kuwaumiza wananchi hasa wanyonge kwa sababu utaathiri shughuli zao za kujipatia kipato.

"Lita ya petroli 3,001 ni kubwa sana maana nishati hii ni muhimu hasa katika masuala ya usafirishaji na uzalishaji viwandani," alisema.

Ali Juma dereva wa daladala alisema kupanda kwa bei ya mafuta huku bei ya usafiri wa daladala kubaki kuwa shilingi 500 ni hasara kubwa kwao.

Hivyo, aliitaka serikali kufanya utaratibu wa kufidia gharama za ununuaji wa nishati hiyo ili kuwapunguzia wananchi gharama za ukali wa maisha.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Frank Nyabundege (katikati), Kaimu Mkurugenzi wa Biashara na Mikopo, Afia Sigge (kushoto) na Mkuu wa Kitengo cha Rasilimali Watu na Utawala, Noelah Ntukamazina, wakikata keki ikiwa ni ishara ya ufunguzi wa Wiki ya Huduma kwa Wateja jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC Kaskazini Unguja akemea vitendo viovu vinavyoharibu utalii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, amepiga marufuku vitendo viovu vinavyoharibu sekta ya utalii ikiwamo kucheza mpira katika fukwe.

Aliyasema hayo jana baada ya kupokea malalamiko ya wananchi wa Kijiji cha Nungwi katika mkoa huo, ikiwa ni sehemu ya kuhitimisha mikutano yake ya kusikiliza kero za wananchi.

Awali wananchi hao walisema uchumi wa nchi unategemea utalii na Kijiji cha Nungwi ni kitovu cha utalii lakini kuna vitendo viovu vinavyofanyika ambavyo vinaharibu utalii.

Alisema miongoni mwa vitendo hivyo ni vitendo vya wizi dhidi ya watalii wanaofika kijijini hapo, akisema ni jambo ambalo halileti taswira nzuri katika sekta ya utalii.

Machano alisema: "Wiki moja iliyopita tumewakamata vijana sita kwa makosa ya kuwapora na kuwaibia watalii waliofika kufanya utalii eneo hili wakiwa katika fukwe."

Aidha, alivitaka vitendo vingine ni usafirishaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya kwa vijana ambavyo vinahatarisha maisha yao na kuharibu zana ya utalii.

Pamoja na mambo mengine, alitaja kero zingine ambazo zimekuwa ni kero kwa watalii wanaofika eneo hilo ni uchezaji wa mpira wa miguu katika fukwe, akisema moja ya kivutio cha watalii wanaofika kijjini hapo ni fukwe.

"Uchezaji wa mpira katika fukwe ni kero kubwa maana mpira unapopigwa shuti huingia mpaka katika sahani ya chakula wakati watalii wakiwa wanapata chakula wakiwa katika fukwe lakini pia ni kero kwa wafanyabiashara," alisema.

Sheha wa Nungwi Banda Kuu, Haji Khamis Haji, alisema mkoa huo kivutio kikuu cha utalii ni fukwe, hivyo ni vyema kuzilinda na kuzihifadhi ili ziwe safi.

Khamis Haji alisema: "Kama kweli tunataka utalii tusafishe fukwe zetu maana ni chafu na itafikia hatua ya watalii tutawakosa."

Naye Mkuu wa Mkoa huo, Ayoub Muhammed Mahmoud, aliwataka wananchi wa kijiji hicho kuandaa sheria ndogo za kijiji ambazo zitawaadhibu wale wote wanaokiuka maadili na kuharibu sekta utalii.

Hivyo, aliwataka wananchi hao kuwa na umoja na ushirikiano katika malezi ya pamoja ili kuwa na jamii bora inayozikatia mila, silka na desturi.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Kaskazini Unguja, Daniel Shila alisema Jeshi la Polisi litaendelea kushirikiana na wananchi katika kuimarisha ulinzi na usalama katika mkoa huo ili kuendelea kupokea watalii wengi.

# Tanzania mwenyeji mkutano wafugaji nyuki

**Na Maulid Mmbaga**

TANZANIA imechaguliwa kuwa mwenyeji wa mkutano wa kimataifa wa ufugaji nyuki 50 Apimondia 2027, kwa niaba ya bara la Afrika ambao unatarajiwa kufanyia 2027 jijini Arusha, ikielezwa kuwa utaleta mapinduzi na manufaa makubwa kwenye sekta ya asali nchini.

Apimondia, ambayo ni Shirikisho la Kimataifa la Vyama vya Wafugaji Nyuki, ni shirika la kimataifa ambalo mamlaka yake ni kukuza ufugaji huo na kila kitu kinachohusiana nacho.

Tanzania ilishinda nafasi hiyo kwa kupata zaidi ya asilimia 60 ya kura na kuzishinda nchi nyingine zilizotaka kupewa nafasi ya kuwa mwenyeji wa kongamano hilo zikiwamo China, Dubai na Togo.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Rais wa Shirikisho la wafugaji Nyuki Kanda ya Afrika, David Mukomana, alisema malengo makuu ya Apimondia ni kuwezesha ubadilishanaji wa taarifa na mijadala ambayo wafugaji wa nyuki, wanasayansi, wafanyabiashara wa asali, mawakala wa maendeleo, mafundi na wabunge wanakutana kusikiliza, kujadili, kujifunza na kubadilishana uzoefu.

"Ilikuwa ni furaha kubwa kuona uungwaji mkono sio tu kutoka kwa wajumbe wengine wa Afrika bali kutoka kwa wadau kutoka mabara mengine wanaotaka kuiona Tanzania ikipata nafasi ya kuwa mwenyeji wa hafla ya kimataifa ya ufugaji nyuki.

"Cha kufurahisha juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan tayari zilishafungua milango kupitia Tanzania Royal Tour ambayo kaulimbiu yake haikuwa na uhusiano wowote na ufugaji nyuki bali kuitangaza Tanzania kama kivutio cha utalii," alisema Mukomana.

**FAIDA**

Aliongeza kuwa baadhi ya faida za moja kwa moja za kuwa na kongamano nchini Tanzania ni kufikika, akisema wafugaji nyuki wa ndani watapata fursa ya kuhudhuria vikao vya bunge, wanachama wa EAC na SADC kupata mkutano huo na chaguzi za kuunganishwa kwa anga.


Pili ni gharama za usafiri ambazo zitakuja nchini, ya tatu ni kufanya biashara kama maonyesho ya asali, kutafuta vifaa, mikutano, fursa za kuongeza thamani ya bidhaa za mizinga, hoteli kupata wageni na kuingiza kipato, biashara ya vifaa, sanaa na utamaduni, ziara za kiufundi na kutembelea tovuti za watalii.

Ya nne ni elimu, maendeleo na mazingira, kama nafasi za kazi kwa watoto, utafiti na uvumbuzi katika ufugaji nyuki, uhifadhi wa mazingira, utatuzi wa migogoro ya wanyamapori na binadamu na utambuzi wa mifumo ya ufugaji nyuki Afrika.

Aidha, alisema kwa sababu hizo Shirikisho la Kanda ya Afrika lilivutiwa kuzungumzia kazi kubwa iliyofanywa na serikali na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) katika kuleta mkutano mkuu wa kimataifa wa kilimo na mifugo nchini Tanzania na kuweka msingi wa fursa kubwa za biashara kwa wajasiriamali.

Pia alibainisha kuwa historia ya Tanzania katika ngazi ya kimataifa ilianza mwaka 1986 wakati ilipokuwa mwanachama wa Apimondia na hatimaye kuwa mwenyeji wa kongamano la kwanza la Apimondia kuhusu Ufugaji Nyuki Afrika iliyofanyika Novemba 2014 mjini Arusha, ambalo lilileta kujulikana kwa umuhimu wa ufugaji nyuki. Na kukuza uchumi wa Tanzania.

Mwenyekiti Mtendaji wa kampuni za PMM zinazojihusisha na masuala ya asali Dk. Judith Mhina, aliishukuru serikali na kueleza kuwa mafanikio hayo yametokana na jitihada za Rais Samia katika kuitangaza Tanzania.




Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja wa Kampuni ya Simu za Mkononi ya Airtel Tanzania, Adriana Lyamba, akikabidhi zawadi ya king'amuzi cha intaneti kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza, Elikana Balandya (kushoto), katika hafla ya maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja mjini Mwanza jana. **NAMPIGAPICHA WETU**

# Mwenyekiti bodaboda taifa avunja uongozi tuhuma kula rambirambi

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

SAKATA la mgogoro baina ya viongozi wa Chama cha Waendesha Pikipiki 'bodaboda' wilayani Geita (CHAMWAPITA) na wanachama wa umoja huo limezidi kuchukua sura mpya baada ya mwenyekiti wa chama hicho taifa, Michael Haule, kuwasimamisha viongozi.

Waliosimamishwa ni pamoja na mwenyekiti na katibu kutokana na tuhuma za ubadhirifu wa fedha za rambirambi zilizochangishwa baada ya kifo cha dereva bodaboda mwenzao, Abel Dotto.

Mwenyekiti huyo alisema amefikia hatua hiyo baada ya maandamano ya wanachama wakiwa na mwili wa mwenzao katika ofisi za uongozi huo na kupokea malalamiko kutoka kwa baadhi yao wakiutuhumu uongozi huo kula michango ya rambirambi.

Kadhalika, alisema tuhuma nyingine ni kushindwa kuwasilisha kwa wakati fedha za wafiwa pamoja na kutokuwasomea wanachama hao mapato na matumizi.

Mwenyekiti alivunja uongozi huo akiwa kwenye kikao maalumu kilichoketi wilayani hapa na kueleza kuwa ameunda kamati ya kuchunguza tuhuma hizo.

Alifafanuwa kuwa chama hicho kimesajiliwa chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa lengo la kusimamia na kutetea haki na maslahi ya bodaboda nchi nzima na kwamba chama hicho sio cha kufa na kuzikana.

Pia amewaagiza wanachama wote nchini waliojiwekea utaratibu wa kuchangishana fedha wanapopata msiba kuweka utaratibu wa kuwasilisha fedha hizo kwa wafiwa kabla ya maziko.

Mwenyekiti wa chama hicho Mkoa wa Geita, Carlos Ndailagiwe, alisema fedha za mchango wa mwanachama anapopata msiba na uchangishaji hufanywa na viongozi wa maegesho wakishirikiana na kamati ya maafa ambayo inasimamiwa na viongozi wa wilaya.

"Hakuna sehemu ambayo uongozi wa mkoa tunahusika kuchangisha fedha hiyo, pia utaratibu wa kuchangishana fedha hizo wanachama wenyewe wamejiwekea na upo kwenye kata nne za halmashauri ya mji wa Geita si kwa wilaya nzima wala mkoa," alisema Carlos.

Baadhi ya wanachama hao, Salvatory Teopard na Respicius Bonevetura, walisema viongozi hao wamekuwa wakichangisha fedha za rambirambi na kuzitafuna wakati mwingine kutozi-wasilisha kwa walengwa kwa wakati.

Mwenyekiti wa chama hicho Wilaya ya Geita, Daniel Dotto, alisema kamati yake ya maafa ilikusanya Sh. 800,000, lakini wanachama hawakukubaliana na taarifa hiyo na kuamua kuchukua mwili na kupeleka ofisini wakiwatuhumu kula fedha zao.

# Wanufaika TASAF watakiwa kuanzisha miradi

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

KAIMU Mkurugenzi Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Shadrack Mziray, amesema wanufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini wanatakiwa kuthamini fedha wanazowezeshwa na kuzitumia kujikwamua kwa kuanzisha miradi midogo ili kutoa nafasi kwa wengine kufikiwa.

Mziray amesema walengwa wanatakiwa kuthamini serikali ilivyowekeza fedha kwenye mpango huo ikilenga kuondoa umaskini na kuwezesha watoto waliokuwa wanakwama kuendelea na masomo kwenda shule kama wengine.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki mjini Bagamoyo wakati wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za viongozi wakuu wa kitaifa kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar, walipotembelea wanufaika wa TASAF.

"Mpango ulikuwa uishe mwaka huu, lakini umeongezwa muda na Sh. bilioni 400 zimeongezwa kwenye mpango huo, ninachowaomba ndugu zangu tuthamini fedha hizi na kazi nzuri inayofanywa na serikali ili lengo lifikiwe," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Machanu Othman, amepongeza utekelezaji wa mpango huo kutokana na miradi mbalimbali iliyofanywa na wanufaika kupitia fedha za TASAF.

Alisema walengwa wanatakiwa kutumia vizuri fursa ya mpango huo kubadilisha maisha yao na endapo watafanya vizuri wakipeleka maombi ya miradi mipya itapitishwa.

Mmoja wa wajumbe wa kamati hiyo kutoka Zanzibar Abdallah Wadi, alipongeza wanufaika wa Mpango huo walivyotekeleza miradi kupitia fedha za TASAF jambo ambalo linaonyesha maendeleo yanavyopatikana kwa kuondosha umaskini.

Mratibu wa TASAF Mkoa wa Pwani, Roseline Kimaro alisema vipo vikundi vilivyoanza kujitoa kwenye mpango kutokana na maisha yao kuimarika.

Katika Wilaya ya Bagamoyo kipindi cha 2023/2024 vijiji 24 vimeibua miradi 31 ambayo inaendelea kutekelezwa na walengwa 1,345 hadi kukamilika itagharimu Sh. milioni 322.8.

HABARI KIMATAIFA

# Mapigano yaendelea Israel, 200 wauawa

**JERUSALEM,** Israel

TAIFA la Israel limeendelea kuwa katika hali mbaya baada ya Hamas kuishambulia nchi hiyo kwa makombora mfululizo ambayo idara ya usalama haikuweza kuyazuia, huku yakisababisha vifo vya watu 200 na 1,000 kujeruhiwa.

Inaelezwa kuwa mashambulizi hayo yalifanyika juzi na waliosababisha waliwateka raia na wanajeshi.

Ripoti iliyotolewa jana na Jeshi la Israel iliishutumu Hamas kwa kufanya mauaji ya raia. Huku majibu ya jeshi la anga la Israel yakisababisha vifo vya takribani watu 232 huko Gaza.

**Ripoti iliyotolewa jana na Jeshi la Israel iliishutumu Hamas kwa kufanya mauaji ya raia. Huku majibu ya jeshi la anga la Israel yakisababisha vifo vya takribani watu 232 huko Gaza.**

Kwa mujibu wa msemaji wa jeshi, wanajeshi wa Israel waliendelea na mapigano katika maeneo 22 dhidi ya mamia ya watu wenye silaha ambao waliivamia Israeli.

Alisema mashambulio ya Hamas yameitikisa Israeli hali ambayo si ya kawaida, akieleza kuwa roketi za kwanza zilizorushwa kutoka Gaza, ziliangukа saa 6:30 asubuhi na wakati jeshi la anga la Israel likijibu kwa kushambulia kwa makombora Ukanda wa Gaza, bado nchi hiyo ilikuwa katika hali ya tahadhari.

Luteni Kanali Richard Hecht, msemaji wa jeshi la Israel, alithibitisha kwamba bado kuna maeneo 22 ambayo wanapigana na magaidi waliokuja Israel kwa ndege, kwa nji ya bahari na nchi kavu.

Akibainisha kuwa bado kuna mamia ya wanamgambo walioingia kwenye ardhi ya Israel.

Mwandishi wa RFI, Emmanuelle Elbaz alisema "katika maeneo ya kusini mwa jiji, mapigano yanaendelea. Jeshi limewakamata magaidi kadhaa wa Hamas, lakini raia wengi bado wamechukuliwa mateka majumbani mwao.

"Raia wamepigwa na mshangao mkubwa, huku wengine wakionekana kuwa na hasira, wakitazama televisheni na mitandao ya kijamii ambako picha za kustaajabisha za raia na wanajeshi wakichukuliwa mateka kwa nguvu hadi Gaza zinazunguka bila kikomo.

Kwa upande wa kisiasa, kiongozi wa upinzani, Yaïr Lapid, amependekeza serikali ya dharura. Pendekezo lililochukuliwa na Likud, chama tawala cha Waziri Mkuu Netanyahu, chama hiki kinasema kiko tayari kuunda serikali pana ya dharura.

Alisema mazungumzo yanaendelea usiku wa jana, huku maonyo ya roketi yakiendelea kusikika na milipuko mikubwa huko Tel Aviv.

Na kwamba jana ilipaswa kuwa siku ya wanafunzi kurejea shuleni, lakini shule zitaendelea kufungwa kutokana na maafa hayo.

Mwandishi Sami Boukhelifa, alisema katika eneo la Sderot, linalopakana na Gaza, pia hali sio nzuri, "Jeshi la anga linatekeleza mashambulizi ya anga. Urushaji wa roketi unaendelea. Roketi hizi zinarushwa kutoka Gaza na kunaswa katika anga ya Israel na kifaa cha kuzuia makombora cha Iron Dome. Baadhi huanguka kwenye maeneo yenye makaazi na kusababisha moto. **RFI**



Kikosi cha zimamoto kikiuzima moto uliotokana na mashambulizi. **PICHA: MTANDAO**

# IOM na UNHCR waiomba Pakistan kusitisha mipango

**ISLAMABAD,** Pakistan

MASHIRIKA ya Umoja wa Mataifa ya wahamiaji na ulinzi wa wakimbizi (IOM na UNHCR) yametoa wito wa pamoja kwa Pakistan kusitisha mipango yake ya kuwafukuza wahamiaji wa Afghanistan wasio na vibali, yakionya kuwa wanaweza kuwaweka hatarini wakirudi Afghanistan.

Wito huo ulitolewa jana baada ya Pakistan kuamuru siku chache zilizopita kwamba wahamiaji wote waishio nchini humo kinyume cha sheria, wakiwamo raia milioni 1.7 wa Afghanistan, waondoke ifikapo Novemba mosi mwaka huu au wafukuzwe na kurejeshwa nchini mwao.

Inaelezwa kuwa familia nyingi tayari zimeondoka kwenda Afghanistan ili kuepuka kukamatwa na kufukuzwa kwa nguvu, huku Wizara ya Habari ya Pakistan ikitoa taarifa ya kila siku kwa wale wanaohusika na sera hiyo kwamba siku zao za kukaa nchini humo zinakaribia kumalizika.

Taarifa ya pamoja ya Shirika la Kimataifa la Uhamiaji na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi, ilisema "Afghanistan inapitia mzozo mbaya wa kibinadamu pamoja na changamoto kadhaa za haki za binadamu, hasa kwa wanawake na wasichana." **VOA**

# Mbunge ahukumiwa kifo DRC

**KINSHASA,** DRC

MBUNGE ambaye ni mmiliki wa kampuni ya kimkakati ya uchimbaji madini, amehukumiwa kifo mjini Kinshasa na mahakama baada ya kupatikana na kosa la kuwa na uhusiano na kundi la waasi la M23 na uhaini nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Inaelezwa kuwa adhabu ya kifo mara nyingi hutolewa nchini DRC, lakini haijatumika kwa miaka 20 na inabadilishwa kwa utaratibu kuwa kifungo cha maisha.

Pia ilielezwa kuwa mwezi Agosti, mwendesha mashtaka wa umma aliomba kifungo cha maisha jela dhidi ya Édouard Mwangachuchu, 70, aliyechaguliwa kutoka Masisi katika mkoa wenye matatizo wa Kivu Kaskazini.

Jenerali Robert Kalala, jaji kiongozi wa Mahakama Kuu ya Kijeshi, alisema mahakama haikumpunguzia adhabu mtuhumiwa huyo, ambaye hakuwapo wakati hukumu hiyo ilipotangazwa, ikielezwa kuwa alipatikana na hatia ya kumiliki silaha kinyume cha sheria na zana za vita, kushiriki katika harakati za kundi la waasi la M23 na uhaini.

Kundi la M23, ni kundi la waasi ambao wengi wao ni kutoka jamii ya Watutsi ambao na kwa madai ya Kinshasa, kutokana na msaada kutoka Rwanda, wameteka maeneo makubwa ya mkoa wa Kivu Kaskazini tangu mwisho wa mwaka 2021.

Mwangachuchu alikamatwa mnamo Machi mosi huko Kinshasa na kwamba alizuiliwa kwanza huko Makala, gereza kuu katika mji mkuu wa Kongo, kisha akahamishiwa katika jela ya kijeshi ya Ndolo ambapo alisikilizwa mara thelathini kuhusiana na kesi yake.

Mshtakiwa mwenzake, Robert Muchamalirwa, ofisa wa polisi mwenye cheo cha Kepteni aliyeshtakiwa kwa kukiuka maagizo aliondolewa mashtaka na mahakama ikaamuru aachiliwe.

Upande wa utetezi wa Mwangachuchu ambaye uliomba kuachiwa huru, ulitangaza nia yake ya kukata rufani katika Mahakama ya juu zaidi. Huku wakili Thomas Gamakolo akishutumu uamuzi usio wa haki, uliochochewa na mambo ambayo hayahusiani na sheria.

Kulingana wa wakili Thomas Gamakolo, uamuzi huo ni jaribio linalotokana na chuki za kikabila na dhana.

Hatujaweza kudhihirisha kwamba Mwangachuchu ana uhusiano na Rwanda, lakini kwa sababu ya Ututsi wake, tumeanzisha dhana ya hatia ni vigumu sana leo katika nchi yetu kuitwa Mtutsi au kutoka jamii ya Watutsi," alisema.

# REKODI MBILI ZA MASHUJAA FC LIGI KUU ZAZIMWA RASMI

**Na Adam Fungamwango**

KIPIGO cha bao 1-0 ilichokipata Mashujaa FC dhidi ya maafande wenzao wa JKT Tanzania kwenye Uwanja wa Kambarage, Shinyanga katikati ya wiki, kimehitimisha rekodi nzuri ya timu hiyo kutopoteza mechi na kutoruhusu bao lolote kwenye Ligi Kuu Tanzania.

Kabla ya hapo, ilikuwa imecheza mechi nne, ikishinda mbili na sare mbili, kisha ikakwama katika mechi hiyo ya raundi ya tano.

**Timu hiyo iliyoanza kucheza Ligi Kuu msimu huu, ilianza ligi kwa kuifunga Kagera Sugar mabao 2-0, Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma, kabla ya kulazimishwa sare nyumbani dhidi ya Geita Gold na ikaisasambua Ihefu mabao 2-0 hapo hapo Kigoma.**

Baada ya mechi tatu za nyumbani ikaenda mkoani Lindi na kuilazimisha suluhu Namungo Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa, na mwisho wa siku ikapoteza mechi ya tano dhidi ya JKT Tanzania.

Katika mechi zote hizo, Mashujaa pia ilikuwa hajaruhusu bao lolote, hivyo rekodi zake mbili zikavunjwa kwa wakati mmoja.

"Tulichoka, tulifika Shinyanga siku moja kabla ya mechi kutoka Mtwara, hivyo uchovu umewaathiri sana wachezaji wangu, lakini ndiyo mpira, niwapongeze sana wapinzani wetu JKT Tanzania walikuwa bora, tunarudi kwenda kujipanga," alisema Kocha Mkuu wa Mashujaa, Mohamed Abdallah 'Bares.'

Mashujaa na Yanga ndizo zilikuwa timu pekee ambazo zilikuwa hazijapoteza mechi na kutoruhusu wavu wao kuguswa, lakini zote zilishindwa kuendeleza rekodi zao katikati ya wiki.

Wakati Mashujaa ikiruhusu bao moja dhidi ya JKT Tanzania, Yanga iliruhusu mabao mawili dhidi ya Ihefu SC, ikifungwa mabao 2-1, zote mbili zikipoteza mechi zao kwa mara ya kwanza msimu huu na kufanya timu zote 16 kuruhusu wavu kuguswa.

Hata hivyo, Simba na Azam zinabaki kuwa timu ambazo hazijapoteza mechi yoyote msimu huu, lakini kwa Wekundu wa Msimbazi hao, inategemeana na matokeo yake ya jana dhidi ya Singida Fountain Gate FC, uliopigwa katika Uwanja wa Liti mkoani Singida.



Stephane Aziz Ki (wa pili kulia), akipongezwa na wachezaji wenzake baada ya kuifungia timu yake bao la pili wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 3-0 ugenini dhidi ya Geita Gold FC, mechi ikipigwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza juzi. **PICHA: PIGAPICHA WETU**

# *TPBRC kugeukia mabondia wa kike*

**Na Shufaa Lyimo**

KAMISHENI ya Ngumi za Kulipwa nchini (TPBRC), imeweka wazi mikakati yake katika mchezo huo, ikitangaza kuwa itahakikisha inainua vipaji vya mabondia wanawake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Kamisheni hiyo, George Silas, alisema lengo lao ni kupata idadi kubwa ya mabondia wa kike ili weweze kucheza mapambano makubwa na kuileta nchini mikanda kama ilivyokuwa kwa upande wa wanaume.

"Tutahakikisha kila pambano linalochezwa lazima liwepo la wanawake ili kupata mabondia wengi wanawake ambao watakuwa na uwezo wa kucheza mapambano makubwa na kuwa mabingwa," alisema Silas.

Aliongeza kuwa kuna mabondia wengi wanawake wana vipaji isipokuwa wanashindwa kufika mbali kutokana na kukosa watu wa kuwaunga mkono.

Mbali na hilo, alisema muda wowote kuanzia sasa watatoa maamuzi rasmi ya tukio lililomfanya bondia Hassan Mwakinyo kugomee pambano lililokuwa lifanyike Septemba 29, mwaka huu, dhidi ya mpinzani wake, Julius Indongo kutoka Namibia.

"Mwakinyo tayari ameleta vielelezo vyake kwa nini alishindwa kupanda ulingoni pamoja na mwandaaji wa Paf Sports Promotion, hivyo muda wowote tutawaeleza Watanzania maamuzi tuliyoyachukua ili wajue kinachoendelea na maagizo tuliyopewa na Baraza la Michezo la Taifa (BMT) ya kupeleka maelezo, tayari tumeshatekeleza," alisema Katibu huyo.

## TMA yaichinja Mbuni Arusha Championship

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya TMA ya Arusha juzi ilipanda kileleni mwa msimamo wa Ligi ya Championship, baada ya kuichinja Mbuni FC pia ya huko kwa bao 1-0, katika mechi kali ya 'dabi ya Monduli' lililochezwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini humo.

Bao lililoipa ushindi TMA liliwekwa wavuni na Abdulaziz Shehame, dakika mbili kabla ya mapumziko na likadumu mpaka dakika 90 zinamalizika.

Ushindi huo unaipeleka TMA juu ya kilele cha msimamo ikiwa na pointi 11, ikicheza mechi tano, kushinda tatu na sare mbili.

Nayo Timu ya Fontaine Gate Academy Talents iliamka kutoka usingizini na kuichapa Polisi Tanzania bao 1-0, mechi ikipigwa Uwanja wa Ushirika, Moshi mkoani Kilimanjaro.



FGA Talents ambayo ilicheza mechi yao ya kwanza baada ya kumtimua kocha Fulgence Novatus kutokana na matokeo mabovu, ilipata bao pekee dakika ya tatu ya mchezo likiwekwa wavuni na Jimmy Simba.

Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, John Tamba (pichani), alisema kupoteza kwa mechi hiyo kunatokana na wao kupoteza nafasi nyingi za kufunga.

"Vijana wamejitahidi kadri ya uwezo wao, lakini tumepoteza nafasi nyingi za kufunga, hili ndilo tatizo letu, tunaenda kulifanyia kazi," alisema Tamba.

Pia alisema wachezaji wa FGA Talents walionekana kupambana zaidi ili kila mmoja kumwaminisha kocha wao mpya kuwa ana uwezo wa kuanza mechi.

"Hii huwa inatokea sana kocha anapokuwa mpya, lakini haya yote yamepita, tunaenda kuangalia makosa yetu," alisema Tamba.

Helbert Lukindo aliipatia Biashara United bao pekee dhidi ya Stand United, mechi ikichezwa Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara, na Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, Cosmopolitan ilipata ushindi wake wa kwanza kwenye ligi hiyo kwa kuifunga Pan African bao 1-0.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### BOWEN MKATABA MPYA

MSHAMBULIAJI wa England, Jarrod Bowen mwenye umri wa miaka 26, alikuwa akihusishwa na Liverpool na Newcastle United, lakini amekubali kusaini mkataba mpya na West Ham. ***(Fabrizio Romano)***

#### SANCHO KWA MKOPO

KLABU ya Juventus huenda ikajaribu kumsajili winga wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 23, kwa mkopo Januari kabla ya kufanya uhamisho huo kuwa wa kudumu msimu ujao. ***(Sun)***

#### MOURINHO NA SAUDIA

KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho, amesema amejitolea kuitumikia klabu hiyo ya Italia, lakini "anashawishika" kwamba siku moja atafanya kazi Saudi Arabia. ***(MBC Misri, Reuters)***

#### ROMA YAKANUSHA RASMI

AS Roma wamekanusha ripoti kwamba wanajiandaa kumfukuza Jose Mourinho na kumleta kocha wa zamani wa Ujerumani, Hansi Flick. ***(ANSA, Football Italia)***

#### JESUS ATAKIWA NAPOLI

NAPOLI inawafuatilia mshambuliaji wa Arsenal na Brazil, Gabriel Jesus, 26, mshambuliaji wa Atletico Madrid na Hispania, Alvaro Morata (30) na mchezaji wa Kimataifa wa Canada, Jonathan David, 23, kama mbadala wa mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen (24), ambaye mkataba wake unamalizika mwaka 2025. ***(Calciomercato)***

#### ZAMBRANO AWINDWA LUTON

MAOFISA wa Klabu ya Luton Town wako Amerika Kusini kwa nia ya kumsajili mchezaji wa LDU Quito, Oscar Zambrano, 19, huku kiungo huyo wa kati wa Ecuador akitajwa kuwa Moises Caicedo ajaye. ***(Sun)***

#### DAVIES AGOMBEWA ULAYA

KLABU za Manchester City na Real Madrid zinatazamiwa kushindania usajili wa beki wa Canada, Alphonso Davies, 22, ambaye mkataba wake na Bayern Munich unamalizika mwaka 2025. ***(Fichajes)***

#### SMITH AFUATILIWA WEST HAM

KLABU ya West Ham inamfuatilia kiungo wa kati wa Arsenal, Emile Smith Rowe, 23. ***(Mail)***

#### KUJIFUNGA BRIGHTON

WINGA wa Japan, Kaoru Mitoma, 26, anakaribia kusaini mkataba mpya wa miaka mitano na Brighton licha ya kuhusishwa na timu kadhaa za Ligi Kuu England.***(Talksport)***

#### NEWCASTLE NA LONGSTAFF

KLABU ya Newcastle United imeanzisha mazungumzo ya kuongeza mkataba wa kiungo wa kati wa England, Sean Longstaff, 25 hadi mwaka 2028. ***(Nicolo Schira)***

#### EVERTON KWA BRANTHWAITE

EVERTON iko mbioni kuafikiana mkataba wa muda mrefu na beki Jarrad Branthwaite mwenye umri wa miaka 21, ambaye anawindwa na Manchester United. ***(Mirror)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# LICHA YA USHINDI TEN HAG AWABWATUKIA MAN UTD

**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag aliwajia juu wachezaji wake wa Manchester United baada ya ushindi wa dakika za lala salama wa mabao 2-1 dhidi ya Brentford akiwaambia, "kama huwezi kustahimili shinikizo, usicheze hapa."

**United ilihitaji mabao mawili ya dakika za lala salama kutoka kwa mchezaji wa akiba Scott McTominay ili kuepuka kichapo cha tatu mfululizo pale Old Trafford kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, Jumamosi.**

Baadaye, Ten Hag alisema timu yake "ilizidiwa" na Brentford katika kipindi cha kwanza na kuwataka wachezaji wake "kudhamiria zaidi."

"Unaposhindwa kuhimili shinikizo, usicheze hapa," alisema Ten Hag.

"Wachezaji ni wazoefu sana, hawa ni wachezaji wa hali ya juu, hivyo wanapaswa kuwajibika.

"Kwenye mpira ni kuliwa au kula.

> ●●● Unaposhindwa kuhimili shinikizo, usicheze hapa, hawa ni wachezaji wa hali ya juu...

Mara nyingi sana katika kipindi cha kwanza cha msimu huu tuliliwa na wapinzani ambao wana njaa zaidi. Hii haiwezi kuendelea kuwa hivi, lazima iondoke. Kila mchezaji anapaswa kujitoa katika kila dakika anapokuwa uwanjani.

"Hilo ndilo hitaji, tumeona msimu uliopita unapata timu iliyodhamiria. Hatukudhamiria kila mara katika mechi, na unapigwa nyundo kwa hilo. Hii lazima libadilike."

Ushindi dhidi ya Brentford umeihakikishia Man United kuelekea mapumziko ya kimataifa wakiwa na matokeo chanya baada ya kufungwa mfululizo na Crystal Palace na Galatasaray.

Wataendelea tena baada ya wiki mbili kwa safari ya kwenda Sheffield United na Ten Hag ameitaka timu yake kutumia mabao ya dakika za mwisho ya McTominay kama kichocheo cha kubadilisha kile ambacho kimekuwa mwanzo wa kusikitisha kwa msimu.

"Hatukuruhusu shuti hata moja na tukapata nafasi na kisha hadithi hiyo hiyo tena, tuliruhusu goli katika dakika mbaya kabisa," Ten Hag alisema.

"Tulianza na hatukuwa kwenye mfumo, zawadi rahisi na ni muhtasari wa msimu wetu. Utoaji kirahisi kama huu, unaadhibiwa kwenye soka la juu. Tuna wachezaji wazuri sana kufanya hivi. Ni lazima tufanye mabadiliko, kuanza upya kwa sababu tunapaswa kuingia katika viwango vya juu.

"Roho ni nzuri, imani ni nzuri na timu iko pamoja. Tumeonesha hivyo, tumeonesha tabia kali. Inaweza kuwa mabadiliko lakini ni juu yetu."

SportPesa
LIVE IN PLA

MECHI KALI
ASEC MIMOSAS
VERSUS
ASI D ABENGOUROU
1 | 1.68
X | 3.09
2 | 5.48

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# MOURINHO AFIKIRIA KUTIMKIA SAUDIA

**ROME,** Italia

KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho, alisema anatarajia kikamilifu kufanya kazi nchini Saudi Arabia siku moja baada ya mwenzake, nahodha wa Ureno, Cristiano Ronaldo, kuongoza kwa kujiunga na Al Nassr, huku wachezaji wengi wakijiunga na timu za Ligi Kuu ya nchi hiyo, Saudi Pro League.

Mourinho alionekana kujiamini kuhamia Saudi Arabia wakati wa mahojiano na Kituo cha Televisheni cha MBC cha Misri, kinachomilikiwa na Saudi MBC Group.

"Nitaenda Saudi Arabia katika muda wa mapumziko, lakini nina hakika kwamba nitafanya kazi huko. Sijui ni lini, lakini nina uhakika wa hilo," alisema Mourinho, ambaye yuko kwenye shinikizo baada ya kuanza vibaya msimu huu pale Roma.

"Hakuna anayejua siku zijazo, lakini kwa hakika nitafanya kazi Saudi Arabia."

Mourinho mwenye umri wa miaka 60, alisema hivi karibu alikataa ofa kubwa kutoka Saudi Arabia ili abaki Roma kwa msimu wa tatu baada ya kuiongoza timu hiyo kutwaa Kombe la Uefa Conference League na kutinga fainali ya Ligi ya Europa.

Lakini Julai iliyopita pia alijiunga na bodi ya wakurugenzi ya Mahd Academy, ambayo inashughulikia ugunduzi wa vipaji nchini Saudi Arabia.



## 'Bellingham alizaliwa kucheza Madrid'

**MADRID,** Hispania

VINICIUS Junior alimsifu Jude Bellingham kama "mchezaji wa ajabu" na kusema kiungo huyo "alizaliwa kuichezea Real Madrid" baada ya raia huyo wa England kufunga mabao mawili katika ushindi wa 4-0 wa klabu hiyo kwenye LaLiga dhidi ya Osasuna Jumamosi.

Bellingham alianza kufunga dakika ya tisa kwenye Uwanja wa Bernabeu, kabla ya kuongeza la pili mapema kipindi cha pili na kufanya kuwa na mabao 10 katika mechi 10 alizoichezea Real Madrid hadi sasa.

Vinicius aliongeza bao la tatu, na Joselu la nne, huku Madrid ikirejea kileleni mwa msimamo wa LaLiga.

"Bellingham alizaliwa kuichezea Real Madrid, kuashiria enzi katika klabu kubwa zaidi duniani," alisema Vinicius akiambia Televisheni ya Real Madrid TV.

"Hebu tumaini muunganisho wetu utadumu kwa miaka mingi, kwamba tutacheza hapa pamoja kwa muda mrefu.

"Nina furaha kucheza na Jude, mmoja wa wachezaji bora kwa sasa, katika umri wake. Sote tuna furaha na mashabiki wanafurahia."

Mabao 10 ya Bellingham katika michezo 10 yanalingana na mwanzo ambao Cristiano Ronaldo - ambaye alikuja kuwa mfungaji bora wa muda wote wa Real Madrid - alipowasili katika klabu hiyo.

CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

# FEI TOTO ATANGAZA MBIO MOJA NA BALEKE LIGI KUU

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuipa timu yake ushindi wa bao pekee ugenini wakati Azam FC ikishinda 1-0 dhidi ya Coastal Union ya Tanga, Kiungo wa Azam FC, Feisal Salum 'Fei Toto', ametangaza vita kwa mshambuliaji wa Simba, Jean Baleke, kwenye mbio za kuwania kiatu cha ufungaji bora Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Fei Toto anashika nafasi ya pili katika mbio hizo akiwa na mabao manne, moja nyuma ya Baleke ambaye amecheka na nyavu mara tano kabla ya mchezo wao wa jana dhidi ya Singida Fountain Gate FC.

**Hata hivyo, Baleke amepata mabao hayo katika mechi tatu alizocheza huku Fei Toto mwenye idadi sawa na nyota watatu wa Yanga, Pacome Zouzoua, Stephen Aziz Ki na Max Nzengeli, wakiyapata kutokana na michezo mitano.**

Akizungumza na Nipashe jana, Fei Toto, alisema wanapambana kusaidia timu yao kufikia malengo ya kusaka pointi tatu kila mechi, lakini pia kuhakikisha anafikia dhamira yake ya ufungaji bora.

Alisema anatambua ushindani uliopo kwenye ligi na anaimani atapambana kuisaidia timu yake kupata matokeo na kutumia vizuri nafasi anayoipata kufunga bao kila mechi ili kufukia malengo yake.

"Malengo ni kuisaidia timu kupata matokeo mazuri kwa kila mechi kwa sababu tunahitaji kutwaa taji la ligi, matarajio yangu pia ni kuwania kiatu cha ufungaji bora kwa msimu huu.

Kuhusu idadi ya mabao anayolenga kufunga msimu huu, alisema: "Siwezi kusema nitafunga mangapi, lakini nimejipanga msimu huu kufunga idadi ya mabao mengi kwa kutumia vizuri nafasi ninazopata katika kila mechi".

Msimu uliopita kiatu cha ufungaji bora kilichukuliwa na nyota wawili, Saidi Ntibazonkiza wa Simba na Fiston Mayele aliyekuwa Yanga kwa sasa Pyramids ya Misri wote wakimaliza na mabao 17.

## Gamondi azitaka pointi 3

INATOKA UK. 24

"Kwa sasa tunaangalia mechi iliyopo mbele yetu, tunafanyia kazi mechi baada ya mechi, nimeona kundi letu, lakini kabla ya kukutana na timu hizo tunakibarua kigumu cha kutafuta pointi kwenye ligi ya nyumbani dhidi ya Azam FC.

"Kundi ni gumu, ukiangalia timu zote ni bora kwa sababu ya kuzifahamu, kasoro Medeama sijaijua vizuri, kwa sasa tunaangalia kilicho kuwa mbele yetu," alisema Gamondi.

Aliongeza kuwa amefurahishwa na kiwango kilichoonesha na wachezaji wake kwa kujua kutumia nafasi walizopata na kufanikiwa kuondoka na alama tatu dhidi ya Geita Gold FC.

Kuhusu kupoteza mechi dhidi ya Ihefu FC, alisema wachezaji walikuwa na fatiki kutokana na wiki moja kucheza mechi tatu na kulazimika kufanya mabadiliko ya kikosi tofauti na mpinzani wao huyo yeye alipata muda mrefu wa kujiandaa.

"Kupoteza mechi moja haina maana tumepoteza malengo yetu, ligi ndio imeanza kuna mechi nyingi mbele yetu na lolote linaweza kutokea, kwa sababu kufungwa na sare ni mambo ya kawaida katika mpira," alisema kocha huyo.

Kuhusu mchezaji wake, Max Nzengeli, alisema ni mchezaji mzuri na anafanya majukumu yake vizuri kwa kushirikiana na wachezaji wenzake kuipa timu matokeo mazuri.



Wachezaji wa Simba wakimpongeza Moses Phiri baada ya kuifungia timu yao bao la ushindi wakati ikiichapa Singida FG mabao 2-1 katika Uwanja wa Liti jana. **PICHA: SIMBA**

## *Simba yarejea kileleni*

INATOKA UKURASA 24

lango la Simba kwa mpira uliopigwa na Duke Abuya ukapanguliwa na Salim, lakini ulimkuta Rupia ambaye alirudisha langoni kipa akiwa chini, mfungaji akaukwamisha wavuni kiulaini licha ya kuzongwa na mabeki.

Kwa matokeo hayo Simba inafikisha pointi 15, mabao 14 huku ikiwa imeruhusu mabao manne, Singida ikibaki na pointi tano kwa mechi tano ilizocheza.



## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 09/10/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2055 | Leixoes SC U23 vs SP. Braga U23 | 3.30 | 3.40 | 1.92 |
| 14:30 | 1104 | Suzhou Dongwu vs Dongguan Guanlian | 2.86 | 3.01 | 2.40 |
| 15:00 | 3261 | Bidco United vs Bandari | 3.58 | 2.91 | 2.10 |
| 15:00 | 4176 | Kampaniakos Chalastras vs Asteras Tripolis | 7.93 | 4.48 | 1.33 |
| 16:00 | 1172 | NK Dubrava vs Solin | 2.00 | 3.27 | 3.27 |
| 16:00 | 3918 | FK Novi Sad vs FK Mladost Gat | 3.45 | 3.05 | 2.00 |
| 16:00 | 5782 | FK Graficar Beograd vs FK Smederevo | 1.88 | 3.23 | 3.73 |
| 16:10 | 3021 | Dubba Al-Husun vs AL Jazira AL Hamra | 1.46 | 4.45 | 5.05 |
| 16:15 | 2482 | AL Arabi vs Al-Hamriyah | 1.94 | 3.64 | 3.13 |
| 16:30 | 1316 | Fajr Sepasi vs Khosheh Talaei | 1.66 | 3.15 | 5.00 |
| 16:30 | 2810 | FK Tyumen vs Torpedo Moscow | 2.62 | 3.02 | 2.52 |
| 17:00 | 1599 | Boca Jrs vs CA Central Cordoba SE Reserve | 1.42 | 3.60 | 7.20 |
| 17:00 | 4229 | Newells Old Boys vs Rosario Central Reserve | 1.94 | 3.20 | 3.40 |
| 17:00 | 4413 | AL Hashemeya vs Sama AL Sarhan | 1.94 | 3.20 | 3.45 |
| 17:00 | 4748 | Belgrano de Cordoba W vs Estudiantes de La Plata | 1.36 | 4.27 | 7.53 |
| 17:30 | 1076 | Stade Renard vs Fauve Azur de Yaounde | 2.00 | 2.95 | 3.55 |
| 18:00 | 2744 | San Lorenzo de Almagro W vs CA Independiente W | 1.78 | 3.46 | 4.02 |
| 18:00 | 5377 | Colombe FC vs Sportive de Douala | 2.16 | 2.80 | 3.57 |
| 18:30 | 1664 | Puerto Montt vs CSD Barnechea | 2.02 | 3.31 | 3.31 |
| 18:30 | 2324 | Deportes Recoleta vs Rangers | 1.96 | 3.41 | 3.36 |
| 18:30 | 3139 | ASEC Mimosas vs Asi D Abengourou | 1.68 | 3.09 | 5.48 |
| 19:00 | 1237 | Donn vs Sandefjord Fotball 2 | 4.10 | 4.50 | 1.53 |
| 19:00 | 1451 | Madla vs Sandnes Ulf 2 | 2.17 | 3.70 | 2.55 |
| 19:00 | 1554 | Odds BK 2 vs Fredrikstad FK 2 | 1.42 | 4.90 | 4.70 |
| 19:00 | 2220 | Sandviken vs Stabaek Fotball 2 | 1.74 | 4.30 | 3.20 |
| 19:00 | 3416 | Vindbjart vs Randesund IL | 1.20 | 6.00 | 8.00 |
| 19:00 | 3809 | FK Khimki vs FC Alania Vladikavkaz | 2.49 | 3.07 | 2.61 |
| 19:00 | 4484 | Athletic Bilbao W vs SC Huelva W | 1.64 | 3.56 | 4.78 |
| 19:00 | 4770 | Sprint/Jeloy vs Start 2 | 1.56 | 4.30 | 4.10 |
| 19:00 | 5932 | Zrinjski Mostar vs FK Sloga Doboj | 1.17 | 6.00 | 10.00 |
| 20:00 | 1839 | Canon Sportif vs PWD Bamenda | 1.52 | 3.61 | 6.11 |
| 20:00 | 1951 | FC Helsingor vs Vendsyssel FF | 2.45 | 3.57 | 2.37 |
| 20:00 | 2253 | Elche vs FC Andorra | 1.98 | 3.27 | 3.57 |
| 20:00 | 2470 | Riteriai B vs Vmfd Zalgiris-3 | 1.51 | 4.10 | 4.70 |
| 21:00 | 2548 | Valencia W vs Levante Las Planas FC W | 1.90 | 3.57 | 3.42 |
| 21:00 | 2585 | Universitatea Cluj vs Sepsi Osk | 2.42 | 3.09 | 2.83 |
| 21:30 | 1795 | Pro Vercelli vs Vicenza | 3.56 | 3.40 | 2.02 |
| 21:45 | 1468 | Gubbio vs Carrarese | 2.51 | 3.09 | 2.88 |
| 21:45 | 2465 | Avellino vs Potenza SC | 1.75 | 3.56 | 4.61 |
| 21:45 | 4095 | Arezzo vs Cesena | 4.70 | 3.76 | 1.69 |
| 21:45 | 5013 | Fermana FC vs Perugia | 4.19 | 3.51 | 1.83 |
| 22:00 | 1027 | Villarreal B vs Espanyol | 4.17 | 3.52 | 1.77 |
| 22:00 | 1341 | Vaca Diez vs CD Real Tomayapo | 2.17 | 3.26 | 3.01 |
| 22:00 | 5577 | Burton vs Cambridge Utd | 2.34 | 3.25 | 2.90 |
| 22:15 | 2817 | Avs Futebol Sad vs Penafiel | 1.70 | 3.47 | 4.60 |
| 23:30 | 1174 | Santiago Wanderers vs Deportes Temuco | 2.18 | 3.11 | 3.11 |
| 23:30 | 1313 | San Marcos vs Antofagasta | 2.48 | 3.42 | 2.48 |
| 23:30 | 3523 | Cruzeiro MG U20 vs Fluminense RJ U20 | 2.13 | 3.57 | 2.85 |
| 23:30 | 4587 | CD Santa Cruz vs Deportes Iquique | 2.40 | 3.26 | 2.65 |
| 23:30 | 5012 | Cobreloa vs San Luis Quillota | 1.81 | 3.32 | 4.08 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Oktoba 9, 2023

Nipashe



Mourinho afikiria kutimkia Saudia UKURASA 22

SAFI...



Saido Ntibazonkiza (kushoto), akimpongeza Kibu Denis, kwa kumpa pasi murua aliyoitendea haki kwa kuuzamisha mpira wavuni na kuiandikia Simba bao la kwanza wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Singida Fountain Gate kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Liti mkoani Singida jana. **PICHA: SIMBA SC**

## Gamondi azitaka pointi tatu Azam

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema hataki kuongea lolote kuhusu mechi za hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, badala yake ameweka wazi kuwa akili yake ipo kwenye mchezo unaofuata wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Azam FC, Oktoba 25, mwaka huu.

Amesema baada ya kufanikiwa kupata alama tatu ugenini dhidi ya Geita Gold FC, nguvu zao wanazielekeza kwenye mechi yao dhidi ya Azam FC , kwani wakati wa kuzungumzia mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika, haujafika.

Yanga inatarajia kutumia mechi hiyo kama maandalizi ya michezo ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambapo itaanzia ugenini dhidi ya CR Belouizdad ya Algeria Novemba 25, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana baada ya kikosi cha Yanga kuwasili Dar es Salaam kikitokea jijini Mwanza, Gamondi alisema baada ya kuvuna alama tatu mbele ya Geita Gold FC sasa wanarejea uwanja wa mazoezi kufanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza na kujiandaa kwa mechi ijayo dhidi ya Azam FC.

Alisema muda huu hafikirii mechi za hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, zaidi ya kufanyia kazi kikosi chake kwa ajili ya mechi yao ijayo dhidi ya Azam FC ambayo itakuwa ya ushindani kwa sababu ya kila timu kuhitaji matokeo chanya.

INAENDELEA UKURASA 23

# Simba yarejea kileleni ilipozoea

## Saido, Phiri wafanya kweli Kibu akizidi kung'ara, huku...

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji raia wa Burundi Saido Ntibazonkiza na straika wa kimataifa wa Zambia, Mosses Phiri, jana waliirudisha Simba kileleni, kila mmoja akifunga bao moja na kuiwezesha kutoka kwenye Uwanja wa Liti na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya wenyeji, Singida Fountain Gate FC.

**Haukuwa ushindi mwepesi hata kidogo kwani Singida ilionekana kudhamiria kupata pointi tatu au moja kwenye mechi hiyo, hata ilipocharuka kipindi cha pili.**

Ilibidi mashabiki wa Simba wasubiri hadi dakika nane kabla ya mechi hiyo kumalizika ndipo nyuso zao zilionekana kuwa na furaha pale Phiri alipoukwamisha mpira wavuni baada ya wachezaji wa timu hiyo kugongeana vema.

Ulikuwa ni mpira ulioanzia kwa Shomari Kapombe pembeni winga ya kulia, akauingiza ndani kwa Fabrice Ngoma ambaye alimwekea Phiri aliyekuwa katikati ya wachezaji Biemes Carno na Yusuph Kagoma, lakini aliwazidi ujanja na kuukwamisha wavuni likiwa ni bao la ushindi.

Ni bao la pili kwa Mzambia huyo kwenye Ligi Kuu, baada ya lile alilofunga Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam dhidi ya Dodoma Jiji, Simba ikishinda mabao 2-0.

Singida ilianza kupiga hodi kwenye lango la Simba dakika ya kwanza tu, pale straika wao Mkenya Elvis Rupia alipowazidi mbio mabeki, lakini alipotezwa maboya na Ally Salim aliyetoka haraka na kumbabaisha, hivyo shuti lake likaenda nje.

Iliwachukua Simba dakika 17 kufika kwa mara ya kwanza langoni kwa Singida, pale Kibu Denis alipowalamba chenga mabeki mmoja baada ya mwingine akitokea kwenye wingi ya kulia, akaingia ndani kidogo kabla ya kuachia shuti lililotemwa na kipa Beno Kakolanya na hakukuwa na mchezaji yeyote wa kuumalizia wavuni, kabla ya kuokolewa na Ahmed Waziri.

Kama angetulia, Bruno Gomes angeweza kuipatia Singida bao dakika ya 20, lakini alikuwa na papara akiwa hajakabwa na mchezaji yeyote wa Simba akapiga shuti nje ya eneo la hatari ambalo lilikwenda mikononi mwa Salim.

Dakika moja baadaye Kakolanya alilazimika kufanya kazi ya ziada kupangua shuti kali la Shomari Kapombe ambaye alikuwa ndani kidogo ya eneo la hatari, huku akilazimika kwenda juu dakika moja nyingine baadaye, kuupangua mpira wa krosi ya Kennedy Juma ambayo ilikatika na kutaka kujaa wavuni.

Ntibazonkiza alianza kuwainua mashabiki wa Simba waliokuwa uwanjani alipopachika bao dakika ya 26 kwa shuti kali la mguu wa kulia, baada ya kazi nzuri ya Kibu.

Kibu ambaye alikuwa kwenye kiwango cha hali ya juu kama siku ambayo timu yake ilipocheza dhidi ya Prisons, aliwatoka mabeki wa Singida mmoja baada ya mwingine kwenye wingi ya kulia, akaingia na mpira ndani kidogo na kumwachia mfungaji ambaye alivuta hatua mbili kabla ya kuachia mashine iliyomzidi nguvu Kalolanya.

Lilikuwa ni bao la pili kwa Saido ambaye katika mechi iliyopita dhidi ya Prisons alifunga bao la tatu kwa mkwaju wa penalti, akiiwezesha kushinda mabao 3-1, Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Kipindi cha pili Singida walionekana kuja kivingine wakiongeza kasi na kulishambulia kama nyuki lango la wapinzani wao.

Almanusura wafunge bao la kusawazisha dakika ya 50, lakini Fondon Che Malone alisimama imara akaokoa shuti kwa kichwa na uliporudishwa akaokoa kwa mguu, wakati huo wote kipa Salim alikuwa ametoka langoni.

Kwa mashambulizi mfululizo waliokuwa wakiyafanya wachezaji wa Singida, haikushangaza walipofanikiwa kusawazisha bao dakika moja baadaye kupitia kwa mtokea benchini, Deus Kaseke, akimalizia mpira uliopingwa na Rupia.

Ilitokea purukushani kwenye

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >